Jumamosi Agosti 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581771
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



UKURASA 21
**ARTETA: UBINGWA EPL 2024/25 WA ARSENAL**


**Ummy** Mwalimu atoa neno kutoswa Baraza la Mawaziri UK. 3



**'Matunda,** vyakula vinavyouzwa kando ya barabara ni hatari kwa afya ya walaji'
UKURASA 9

**Serikali** yabaini shida matumizi mabilioni ya CSR migodi ya madini
UKURASA 9

# Mshtuko CCM kumchangia fedha Lissu



• **CHADEMA** yavuta subira, wachambuzi wa siasa wadai "kuna kitu nyuma yake"; mwenyewe asema... *Ukurasa 2*



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Kisongo, Godfrey Kaaya (kushoto), alipofanya ziara ya kukagua ukarabati wa jengo la kupokea wageni wanaowasili na kuondoka, jijini Arusha jana. **PICHA: WOINDE SHIZZA**


BAADA YA SIKU 32 UKURASA 3

## Makonda aonekana, aibukia mradi wa uwanja wa ndege

UKURASA WA 12

## HAMISA MOBETO SASA MWENDO WA MIKOGO

MWANAMUZIKI na mwanamitindo, Hamisa Mobetto, amewakoga watu kwamba mapenzi anayoyapata anajiona tayari amefika peponi...



## Uongozi TRC wacharuka ripoti ya TAKUKURU hujuma mapato ya treni za SGR

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA UWANJANI IKIWAZA TAJI CAF** UK.24 **MAONI,** UK.6

# Ripoti ya TAKUKURU hujuma mapato treni SGR yashtua TRC

**Na James Kandoya**

BAADA ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKUKU) kuanika namna baadhi ya abiria wa treni ya mwendokasi kutolipa nauli sahihi kulingana na safari wanazofanya, Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeeleza mikakati yake kudhibiti hujuma hizo.

Juzi TAKUKURU Mkoa wa Morogoro ilieleza namna baadhi ya abiria wanaotumia SGR wanavyokwepa kulipa nauli sahihi kulingana na safari wanazofanya.

Taasisi hiyo ilisema imebaini baadhi ya abiria wasio waaminifu hasa wanatokea Dar es Salaam kwenda maeneo mengine hasa vituo vya njiani vyenye nauli kidogo kama vile Pugu (Sh. 1,000), Soga (Sh. 4,000), Ruvu (Sh. 5,000) na Ngerengere (Sh. 9,000), treni inapokuwa inakwenda Morogoro.

Nauli ya treni kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni Sh. 13,000 kwa daraja la kawaida na Sh. 21,000 kwa daraja la juu.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano kwa Umma cha shirika hilo, Jamila Mbarouk, akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, alisema tayari baadhi ya watuhumiwa wa vitendo hivi wapo mikononi mwa vyombo vya dola kwa ajili ya mahojiano.

Kuhusu mbinu watakazotumia kudhibiti vitendo hivyo, Jamila alisema kwa safari zote sasa kutakuwa na ukaguzi wa tiketi wa mara kwa mara na abiria atapaswa kuchanja tiketi yake mwanzo na mwisho wa safari.

Vilevile, alisema kuwa kuanzia sasa, hakuna abiria ataruhusiwa kukata tiketi bila kuwa na kitambulisho kinachomtambulisha ili kudhibiti tabia ya baadhi ya abiria kununua tiketi nyingi na kulangua kwa bei ya juu.

"Shirika limechukua hatua hizi ili kudhibiti vitendo viovu vya baadhi ya abiria wanaotumia treni kwa kutolipa nauli sahihi na kulangua tiketi.

"Tumeboresha mfumo wetu wa ukaguzi ambapo sasa abiria atachanja tiketi anapopanda na kushuka na hatapewa huduma ya kununua tiketi kama hana kitambulisho," alisema.

Jamila alisema atakayebainika hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwamo kulipa faini au kupelekwa mahakamani kulingana na sheria itakavyoelekeza.




Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Mlezi wa CCM Mkoa wa Dodoma, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akivishwa vazi la kimila la mkoa huo na machifu, wakati wa mkutano wa viongozi na wanachama wa chama hicho, mkoani humo, jana. **PICHA: OMR**

# Mshtuko CCM kumchangia Lissu

**Na Waandishi Wetu**

UAMUZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kumchangia fedha Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu anunue gari jipya, umeibua minong'ono:

Wachambuzi wa siasa wamesema mwitikio wa Watanzania wengi kumchangia mwanasiasa huyo wa upinzani umeishtua CCM na kuona kuna haja wao pia wamchangie fedha; kufanya hivyo ni fursa kwao kisiasa.

Kwa upande wa chama chake - CHADEMA, viongozi wanavuta subira, wakisisitiza kauli itatolewa baada ya kujiridhisha "kweli CCM wameweka fedha katika akaunti ya Lissu".

Agosti 14 mwaka huu, Katibu wa NEC - Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Amos Makalla, aliendesha harambee ya kumchangia fedha Lissu ili atengeneze gari lake ambalo alikabidhiwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Dodoma Mei 17, mwaka huu.

Ni gari lenye matobo ya risasi za tukio la kushambuliwa kwa silaha za moto Septemba 7, 2017, wakati anajiandaa kushuka nyumbani kwake Area D, jijini Dodoma.

Harambee hiyo ilifanyika kwenye Uwanja wa Furahisha, jijini Mwanza wakati wa mkutano wa hadhara wa Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, Sh. milioni 5.3 zikichangwa.

Mchambuzi wa siasa, Bubelwa Kaiza, alipotafutwa na Nipashe jana kuzungumzia uamuzi huo wa CCM, alisema michango ya kununua gari la Lissu haikuanzishwa na Lissu, bali Watanzania wanaompenda ambao walikubaliana anunue gari jipya badala ya kutengeneza lile lililoshapigwa risasi.

"Wapenzi wake wakaona gari lile liwe historia. Ninachokiona ni kwamba, mwitikio wa watu wanaomuunga mkono Lissu ndio ulioisukuma CCM kumchangia. CCM wameona ni jambo la kisiasa. Katika hali ya kawaida ni jambo zuri," alisema.

Kaiza alisema mchango huo umeipa CCM fursa ya kuwapa wanachama wake wenye mapenzi mema kumchangia kiongozi huyo ambaye ni kada wa CHADEMA.

Mchambuzi wa siasa, Luwaga Kizoka, alisema uamuzi huo wa CCM umeonesha ukomavu wa kisiasa, akisisitiza wanasiasa wanapaswa kupingana kiitikadi na si kujenga uadui.

"Ni hatua nzuri ambazo uongozi wa juu wa chama (CCM) unaendelea kuzichukua kuhakikisha kwamba siasa za maridhiano na kujenga upya zinapewa kipaumbele katika awamu ya sita (Falsafa ya R4 za Rais Samia Suluhu Hassan)," alisema Kizoka.

**KAULI CHADEMA**

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi, Uenezi na Mambo ya Nje CHADEMA, John Mrema, alipotafutwa na Nipashe jana kutaka kujua msimamo wa chama chao baada ya harambee hiyo ya CCM kufanyika, alisema hawawezi kutoa kauli kwa sasa.

Mrema alisema, "hatuwezi kutoa kauli kwa sasa kwa sababu hatujathibitisha kama fedha hizo zimeingizwa kweli katika akaunti ya Makamu Mwenyekiti (Lissu) au la".

Katika mkutano wa CCM ulioendesha harambee kumchangia Lissu, Makalla alisema amesikitishwa na taarifa iliyotolewa na kada wa zamani wa CHADEMA, Mch. Peter Msigwa, kada mpya wa CCM, kwamba, wakati kiongozi wake akipaa na chopa angani na msafara wa magari 15, Lissu amekuwa akitumia gari moja bovu na walinzi wake licha ya hali aliyonayo kiafya.

Makalla alisema Lissu ni ndugu yake na wanatoka mkoa mmoja wa Singida na kuomba waliguswa kumchangia ili gari hilo litengenezwe. Katika harambee hiyo, baadhi ya makada wa CCM, akiwamo Katibu Mkuu Balozi Nchimbi, walichangia na kupata kwa kiasi hicho - Sh. milioni 5.3.

Akizungumza na chombo kimoja cha habari, si Nipashe, Lissu alisema jana kuwa, "Ninawashukuru. Kama nilivyosema, hao waliosema wananichangia, hatukusema ni wana-CHADEMA peke yao, kama nilivyotibiwa, sikutibiwa na wana-CHADEMA peke yao, (CCM) wakichanga nitazipokea, sina sababu ya kukataa."

***Imeandaliwa na Romana Mallya na Restuta James**




Waendesha baiskeli ya magurudumu matatu maarufu guta, wakiwa wamezisheheni mzigo wa mapipa ya plastiki na kuwafanya washindwe kuona nyuma katika Barabara ya Kawawa, Dar es Salaam mapema wiki hii, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Makonda aonekana, aanza na uwanja wa ndege

**Na Beatrice Shayo**

MKUU wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, ameonekana kwa mara ya kwanza katika shughuli rasmi za kiserikali baada ya kuwa kimya kwa siku 32 tangu Julai 14 mwaka huu aliposhiriki kutoa zawadi katika mashindano ya mbio za pikipiki mkoani humo.

Kuliibuka uvumi kuhusu kiongozi huyo licha ya Katibu Tawala Mkoa wa Arusha kutoa ufafanuzi kuwa "Makonda alikuwa likizo".

Baada ya ukimya huo, jana Makonda alionekana rasmi katika shughuli za kiserikali, akiagiza kukamilika kwa haraka ujenzi wa jengo la abiria kwenye Uwanja wa Ndege Kisongo, mkoani Arusha ili kuanza kutoa huduma ifikapo Septemba Mosi mwaka huu.

Makonda aliagiza hayo jana baada ya kufanya ukaguzi wa jengo hilo la abiria ambalo litakuwa na uwezo wa kutoa huduma kwa abiria 1,000 kulinganishwa na uwezo wa sasa wa kutoa huduma kwa abiria 150.

"Nimepata nafasi ya kutembelea uwanja wetu wa Kisongo Arusha na lengo kubwa ni kuona maendeleo ya ujenzi na ukamilishaji ahadi iliyotolewa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) chini ya Rais Samia Suluhu Hassan," alisema.

Makonda alisema kazi inaendelea vizuri na inawapa faraja, akielekeza kazi zifanywe usiku na mchana kukamilisha mradi huo.

"Shauku ya wananchi wa Arusha, shauku ya wageni wetu wa kanda zote, wakiwamo watalii wanatoka Zanzibar, kuja moja kwa moja hadi Kisongo, Arusha kwa muda wowote, iwe ni mchana au usiku," alisema.

Makonda alisema wanatamani kuona uwanja kama unaweza kutumika kwa wageni ambao wana ndege binafsi kutoka kwenye baadhi ya nchi nyingine wanaotaka kwenda mbugani na kupanda Mlima Kilimanjaro.

Alisema taarifa walizozipata kutoka kwa mhandisi, ifikapo Septemba Mosi, jengo hilo litaanza kufanya kazi kutoka kubeba abiria 150 katika jengo la zamani na kuanza kuchukua idadi ya watu 1,000 kwa wakati mmoja.

Alisema jambo hilo lina manufaa makubwa kwa kuwa wanakwenda kuondoa msongamano na usumbufu ambao ulikuwa unajitokeza kutokana na ongezeko la abiria kwenye Uwanja wa Kisongo.

Makonda alisema suala la pili ni kuweka taa kwa kuwa uwanja, ili ufanye kazi kwa saa 24, zinahitajika taa na tayari mkandarasi amepatikana na mkataba umeshatiwa saini, na wanamalizia usanifu.

Alisema mkataba huo ni wa miezi 12 ingawa wamezungumza na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TCAA), ahimize akamilishe kazi yake ndani ya miezi minane.

"Tunahitaji taa ili tukamilishe ndoto ya Watanzania na wananchi wa Mkoa wa Arusha uwanja wao kutumika saa 24, bila kuwa na taa maana yake hatuwezi kuutumia huu uwanja kwa saa 24.

"Kipekee ninamshukuru Rais Samia, serikali kutupatia zaidi ya Sh. bilioni saba kuhakikisha uwanja huu unafungwa taa za kuongoza ndege," alisema Makonda.

Alisema wanaongeza mita 200 hadi 500 ili kuwapo njia pana ili ndege zipaki na kugeuka bila kuwa na shida yoyote.

Alisema Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni na Waziri wa Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa "ni waungwana, watafanya kikao chao cha ndani ili kuwasilisha taarifa kwa viongozi hao waongeze upana wa uwanja".

# Ummy Mwalimu atoa neno kutoswa Baraza la Mawaziri

**Na Romana Mallya**

SIKU mbili baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kumwondoa Ummy Mwalimu katika Baraza la Mawaziri, Mbunge huyo wa Tanga Mjini 'amefunguka', akimshukuru Mkuu wa Nchi kwa kumwamini na kumpa heshima ya kutoa huduma serikalini.

Mara tu baada ya kukabidhi ofisi kwa Waziri mpya wa Afya, Jenister Mhagama, Ummy aliandika katika ukurasa wake wa Instagram maneno ya kumshukuru Rais kwa namna alivyomwamini.

"Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema na baraka zake na kwa kila hatua tupitazo kwa kuwa zimezungukwa na neema zake ikiwamo kupata kibali cha kuitumikia nchi yangu katika nafasi ya Naibu Waziri (2010 - 2015) na Waziri (2015 hadi 2024). Si kwa uwezo au ujanja wangu, bali ni kwa ukuu wa Mungu.

"Pili, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa ninamshukuru Mheshimiwa Rais Samia kuniamini na kunipa heshima ya kuhudumu katika serikali yake katika nafasi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Machi 2021 hadi Januari 2022.

"Na Waziri wa Afya (Januari 2022 hadi Agosti 14, 2024). Asante sana Mheshimiwa Rais kwa imani na heshima kubwa uliyonipatia. Nitaenzi na kuitunza heshima hii daima," aliandika Ummy ambaye amehudumu Baraza la Mawiziri kwa miaka 14.

Aliendelea kueleza kuwa kwamba, kwa muda aliohudumu katika Wizara ya Afya, ameona ari, juhudi na kiu ya Rais Samia ya kuboreshea Watanzania huduma za afya na wametoa mchango wao katika hilo.

"Yapo mengi tumeyasukuma na ambayo yanaendelea kusukumwa. Pongezi za dhati kwa dada yangu, Mheshimiwa Jenister Mhagama kwa kupokea kijiti.

"Sina shaka na uwezo, uzoefu na kujituma kwake katika kufikia malengo tuliyojiwekea pamoja na maono ya Mheshimiwa Rais ya kuhakikisha upatikanaji huduma bora za afya kwa Watanzania. Namtakia heri katika utekelezaji wa majukumu yake mapya," alisema.

Ummy ambaye amehudumu kwa muda mrefu katika wizara hiyo pia ameshukuru viongozi na watumishi wa wizara hiyo, wadau wa maendeleo na asasi za kiraia kwa ushirikiano mzuri waliompatia ambao alisema umewezesha nchi kupata matokeo chanya katika maeneo mbalimbali ya upatikanaji huduma za afya kwa wananchi.

"Shukurani za kipekee ni kwa wapigakura wangu wa Jimbo la Tanga Mjini kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia na kwa uvumilivu wao mkubwa wakati wa utekelezaji majukumu yangu ya kitaifa.

"Asanteni sana wanaKimji. Nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa ufanisi na sasa kwa karibu zaidi katika kuijenga Tanga yetu. Kazi kubwa iliyo mbele yetu sasa ni kutafuta ushindi wa kishindo wa CCM katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025," alisema Ummy.

Baadhi ya wananchi walioandika katika ukurasa wake akiwamo anayejiita Malisa_gj, alimpa hongera pamoja na changamoto mbalimbali zilizoko katika sekta ya afya, akimweleza kwamba alijitahidi kutimiza yale yaliyokuwa ndani ya uwezo wake.

Wakati Susan_mlekia ameandika, "Hongera Odo (mama mdogo), wewe ni kiongozi mahiri na hakika ulijitahidi sana katika sekta ya afya nchini. Asante kwa utumishi mzuri, hakika wewe ni mfano wa kuigwa."

# TFRA yanyatia utoroshaji mbolea nje ya nchi

**Na Moses Ng'wat,** SONGWE

SERIKALI kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetangaza hatua kali zaidi zinazolenga kudhibiti tatizo la utoroshaji mbolea ya ruzuku kwenda nje ya nchi.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Meneja wa TFRA Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Joshua Ng'ondya, alisema mamlaka imeajiri wataalamu katika maeneo ya mipakani watakaohusika moja kwa moja na kudhibiti utoroshwaji mbolea kwenda nje ya nchi kunakofanywa na baadhi ya watu na wafanyabiashara wasio waaminifu.

Ng'ondya alitaja mkakati mwingine ambao utatumika kudhibiti tatizo hilo ni mamlaka hiyo kuingia mkataba wa hati ya makubaliano (MoU) na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA) ili kudhibiti mipaka rasmi.

Alisema mikakati hiyo pia inakwenda sambamba na operesheni mbalimbali za kushtukiza zitakazoendelea kufanywa kwa ushirikiano na mamlaka na vyombo vya ulinzi na usalama ikiwamo kufuatilia wafanyabiashara wanaotiliwa shaka katika mfumo wa mauzo ya mbolea ili kujiridhisha na mwenendo wa mauzo yao.

"TFRA tunakemea kwa nguvu zote vitendo vya hujuma kwa taifa na tumejipanga kweli kweli kuhakikisha yeyote atakayejiingiza katika hujuma za utoroshaji mbolea, anachukuliwa hatua kali ili iwe fundisho kwa watu wengine," alionya Ng'ondya.

> **"TFRA tunakemea kwa nguvu zote vitendo vya hujuma kwa taifa na tumejipanga kweli kweli kuhakikisha yeyote atakayejiingiza katika hujuma za utoroshaji mbolea, anachukuliwa**

Alisema kuwa licha ya serikali kufanya operesheni mbalimbali za kudhibiti utoroshwaji mbolea hiyo ya ruzuku kwenda nje ya nchi, baadhi ya watu wamebadili mbinu za usafirishaji kwa kutoka kutumia malori na sasa husafirisha kwa kutumia magari madogo ya abiria (hiace), bajaji na pikipiki.

Ng'ondya alisema kuwa Jumatatu iliyopita, mamlaka hiyo ilikamata mfanyabiashara Furaha Mwakalengela, akidaiwa kukutwa na mifuko 128 ya mbolea aina ya Urea, aliyokuwa akitorosha kwenda Malawi kwa kutumia hiace yenye namba za usajili T 706 BMK.

Ng'ondya alisema TFRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi lilikamata hiace nyingine yenye namba za usajili T 168 CRS siku hiyo hiyo, ikiwa na mifuko 44 ya mbolea ikitoroshwa kwenda nje ya nchi.

Pia walikamata bajaji zenye namba MC 681 EHR na MC 532 DRN zikiwa na mifuko mitano kila moja na watuhumiwa wa vyombo hivyo vinashikiliwa katika Kituo cha Polisi Tunduma.



Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura, akizungumza na maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali wa Mkoa wa Kilimanjaro jana, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kikazi mkoani humo. IGP Wambura, amewataka kuendelea kutekeleza majukumu yao ya kazi na kuzingatia nidhamu, weledi, uadilifu na kutenda haki kwa wananchi wanaowahudumia sambamba na utekelezaji wa maelekezo ya Tume ya Haki Jinai. **PICHA: POLISI**

# Jeshi la Ulinzi lawapa msaada wanafunzi wenye ulemavu

**Na Ally Hengo**

MIKOA ya Shinyanga, Simiyu na Geita yenye wanafunzi wa kike katika shule maalum zenye uhitaji wa taulo za kike, inatarajiwa kupatiwa taulo za kike kwa ajili ya wanafunzi 300.

Taulo hizo zilizotolewa na Chama cha Akiba na Mikopo cha Ngome kilichoko chini ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi Tanzania. Zimepokewa kupitia Taasisi ya Wenye Ulemavu (DCDO) iliyoko Mbezi, Dar es Salaam.

Akikabidhi msaada huo jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Kanali Aisha Matanza, alisema wameguswa kuona kuna kundi hilo katika jamii ambalo linakabiliwa na ugumu katika kupata vifaa sahihi kuliwezesha kuwa na hedhi salama.

Alisema licha ya majukumu yao ya kiulinzi, haiwazuii kusaidia jamii kama hizo ambazo zina uhitaji mkubwa na kuzitaka taasisi zingine nazo ziguswe.

Meneja wa chama hicho, Luteni Kanali Lucy Chacha, alisema hiyo si mara kwanza kutoa misaada ya aina hiyo hususani kwa watu wenye ulemavu na kupitia taasisi hiyo ya watu wenye ulemavu walishatoa katika mikoa ya Pwani, Tanga na Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa DCDO, Hamisi Uchuro, alishukuru chama hicho kwa ufadhili huo. Alisema licha ya ulemavu wao, wamekuwa wakitafuta misaada mbalimbali ya kijamii kwa kuwa nao walishapitia changamoto za aina hiyo walipokuwa shuleni. Uchuro aliomba jamii na taasisi binafsi kujitoa kwa ajili ya kundi hilo, hasa watoto wa kike ambao wengi wanatoka familia duni zisizo na uwezo wa kuwanunulia taulo za kike kila mwezi ili kuwasaidia.

# ACT: Kutelekeza mkonge na uvuvi kunaleta ufukara

**Na Mwandishi Wetu,** PANGANI

MAKAMU Mwenyekiti ACT- Wazalendo Bara, Isihaka Mchinjita amesema kufa kwa viwanda na shughuli za uchumi katika miji ya Pwani ya Bahari ya Hindi, ikiwamo mikoa ya Tanga, Pwani, Lindi na Mtwara, kumechangia kwa kiasi kikubwa kudumaa kwa uchumi wa miji na wilaya zake.

Alitoa kauli hiyo jana akiwa katika Jimbo la Pangani, Mkoa wa Tanga ikiwa ni mwendelezo wa ziara ya viongozi wakuu wa ACT Wazalendo iliyolenga kuyafikia majimbo 214 Tanzania Bara.

Kiongozi huyo alisisitiza kwamba sera na uamuzi huo umesababisha kuzalisha na kukuza umaskini uliopitiliza kwa wakazi wa Pangani, akiomba wakazi wa Tanga kuachana na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kujiunga na ACT.

Alisema Mkoa wa Tanga ulikuwa kinara wa viwanda na kilimo cha katani kilienda sambamba na viwanda vya uchakataji wa zao hilo na kulinufaisha Taifa.

"Zao la katani hivi sasa limezidi kupata thamani duniani lakini serikali haiweki msisitizo wowote kulifufua au kufufua viwanda vyake.

"Mkoa wa Tanga ulikuwa na mchango mkubwa kutokana na zao la katani, nchi ilikuwa inaongoza kwa uzalishaji katani duniani. Mwaka 1970 Tanzania iliuza nje tani 230,000 lakini mwaka 2023 imezalisha tani 56,732," alisema Mchinjita.

Aliongeza kuwa licha ya kwamba ukanda huo wa bahari unabeba kilomita 1,500 kutoa fursa kubwa katika sekta ya uvuvi, serikali imeipa kisogo sekta hiyo.

'"Kupuuzwa kwa sekta hiyo, pamoja na madhila ya wavuvi wadogo kunyanyaswa na kuonewa, ndio kumepelekea kuongezeka kwa maskani za kahawa na ukosefu wa ajira.

"ACT-Wazalendo inaamini kufufua na kuanzishwa viwanda vya samaki, vitakavyotengeneza ajira kwa wakazi wa Tanga, ni njia ya kukuza uchumi wa Mkoa huo," alisema Mchinjita, akisisitiza kuwapo viwanda hivyo ndio njia pekee ya kunusuru wakazi wa Tanga na maeneo ya ukanda wa Pwani.

Naye Janeth Fusi, Katibu wa Ngome ya Wazee Taifa, alisema amesikitishwa na kitendo cha wanawake wilayani Pangani kutozwa fedha wakati wa kujifungua.

Alisema licha ya serikali kuweka sera ya huduma za bure kwa wajawazito, wazee na watoto, bado kuna wanawake wengi wanaoishi maeneo ya vijijini wanakumbana na adha wakati wa kujifungua na kupata huduma katika vituo vya afya.

"Ni wazi kuwa sera hii ni ulaghai mtupu. Kuna hili suala la wale wanaojifungulia majumbani kutokana na kushindwa kufika hospitali kwa sababu ya mazingira mabovu ya miundo mbinu, wanalazimishwa kulipa fidia ya Sh. 50,000.

"Huyu ni mzazi anataka kusajili mwanawe baada ya kujifungua kwa tabu huko alipotoka, wao wanamtoza fedha ya faini, ninawauliza hizi fedha ni kwa ajili ya nini na manufaa ya nani na inaingia katika mfuko gani?" alihoji Fusi.

Raya Ibrahim Khamis, Naibu Waziri Kivuli wa Migodi na Madini alisisitizia wakazi wa Pangani kuwa Pangani wanayoitaka; Pangani inayotoa suluhu kwa watu wa Pangani, Tanga na Tanzania; Pangani isiyoulizana "Kunani Pangani", inaweza kupatikana kupitia ACT-Wazalendo tu.

Makamu Mwenyekiti Bara na msafara wake wanaendelea na ziara katika Mkoa wa Tanga kwenye Jimbo la Mkinga. Ziara hiyo ikiwa ni awamu ya kwanza kuyafikia majimbo yote 214 Tanzania Bara.

## HABARI KITAIFA

# TAREA yataka wananchi watumie nishati mbadala

**Na Mary Geofrey**

WADAU wa Nishati Jadilifu (TAREA) wameshauri wananchi kutumia nishati mbadala ambayo ni safi kwa mazingira hasa katika maeneo ambako umeme haujafika.

TAREA pia imeshauri matumizi ya bidhaa zilizotengenezwa mahusus kwa nishati mbadala ambazo ni safi kwa mazingira na hazina kelele.

Naibu Katibu Mtendaji wa TAREA, Emma Laswai, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa ushirikiano wa Kampuni za Luminous Power Teknologies na Swaminath Trading zinazoshirikiana kuleta bidhaa za nishati ya jua.

Alisema TAREA iko katika mkakati wa kuhakikisha wananchi wote bila kujali uchumi wao wanafikiwa na huduma ya nishati safi.

Laswai alisema wadau hao wakiwamo Luminous na Swaminath wanazalisha jenereta ambazo hazipigi kelele na kutoa hewa chafu zinazounga mkono juhudi za serikali za kupunguza nishati mbadala.

"Ushirikiano kati ya kampuni ya Swaminath Trading na Luminous ni ushahidi wa kukua kwa teknolojia, soko la nishati ya jua na mazingira bora ya biashara nchini.

"TAREA imejizatiti kuhakikisha ubora wa bidhaa na huduma bora zaidi ili kuhakikisha uendelevu unazingatiwa katika juhudi zetu," alisema.

Makamu wa Rais wa Biashara ya Kimataifa, Luminous Revanand Andhale, aliahidi kupitia ushirikiano huo wataingiza nchini bidhaa zenye ubunifu wa hali ya juu zilizotengenezwa kwa ajili ya soko la Tanzania.

"Tumewaletea Watanzania suluhisho la kudumu la upatikanaji nishati kwao kwa sababu kuna ongezeko la mahitaji ya umeme nchini na tuna imani vitawafaa kwa matumuzi ya kila siku," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Swaminath Group, Mayur Dilesh Solaki, alisema wataleta vifaa vya umeme mbadala vyenye viwango ubora wa kimataifa.

"Ushirikiano huu unaonesha kujitolea kwetu katika kuendeleza teknolojia na kukuza nishati endelevu nchini.

"Tumelenga kuendelea kuwapa wateja wetu suluhisho la muda mrefu kwa vifaa vya kisasa vyenye ubora wa hali ya juu na kwa bei nafuu kulinganishwa na bidhaa shindani," alisema.



Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Dar es Salaam, Songoro Mnyonge (kushoto), akipokea tuzo ya mshindi wa jumla katika Kanda ya Mashariki kutoka kwa Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Hanifa Hamza, wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani jana, iliyotokana na manispaa hiyo kushiriki katika Maonesho ya Wakulima Nanenane mkoani Morogoro, hivi karibuni. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Meya: Bado kidogo Morogoro kuwa Jiji

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Manispaa ya Morogoro imesema imebakiza hatua chache kukamilisha mchakato muhimu wa kufikia vigezo vitatu vya kiserikali vinavyoitaka manispaa kuwa jiji.

Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Pascal Kihanga alisema hayo jana wakati anazungumza na waandishi wa habari ofisini kwake baada ya kutoka kwenye kikao cha robo ya mwisho cha Baraza la Madiwani kilichofanyika mjini hapa.

Kihanga alisema Rais Samia Suluhu Hassan alisema Morogoro kuwa jiji kwa sasa si sahihi, lakini wao kama manispaa wapo katika kiwango kizuri cha kufikia vigezo vya kuwa jiji; wanakaribia kutimiza vigezo vitatu vinavyohitajika.

Alivitaja vigezo hivyo vinavyohitajika manispaa kuwa jiji kuwa ni kiwango cha ukusanyaji mapato, urefu wa barabara za kiwango cha lami na idadi ya watu katika eneo husika.

Alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, manispaa ina jumla watu 471,000 na wanaohitajika ni watu 500,000 kuwa jiji.

Alisema kuwa hivi sasa wana upungufu wa kilometa 22 za barabara za lami ambazo wanatarajia kuzikamilisha hivi karibuni ili kutimiza vigezo vya kuwa jiji na makusanyo ya mapato kwa mwaka ni Sh. bilioni 15; mwakani wanatarajia kuongeza makusanyo na kufikia Sh. bilioni 20 na kuvuka lengo la makusanyo la Sh. bilioni 17.

"Tanga wao ni jiji, wanakusanya Sh. bilioni 17, sisi mwakani tunakwenda kukusanya Sh. bilioni 20, huoni kama tunakwenda kuwa zaidi ya jiji?" alitamba meya huyo.

Meya Kihanga aliomba wananchi kuwa watulivu bila kuvunjika moyo wakitambua kuwa manispaa inaendelea kutimiza vigezo.

Hivi karibuni Rais Samia alizuru Morogoro kwa siku sita. Akizungumza na wananchi kwenye Uwanja wa Jamhuri, Mbunge wa Morogoro Mjini Abdulaziz Abood alimwomba kuruhusu manispaa kuwa jiji; naye alisema Manispaa ya Morogoro haijafikia hadhi ya kuwa jiji.

# TCRA yadhamini wanafunzi watano mashindano hisabati

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imedhamini wanafunzi watano wa Kitanzania watakaoshiriki mashindano ya nchi za Afrika ya Hisabati yanayofanyika Chuo Kikuu cha Witwatersland, Afrika Kusini.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari aliyasema hayo juzi wakati anazungumza na waandishi wa habari kuhusu udhamini huo.

Alisema hatua hiyo ni sehemu ya kuendeleza stadi za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) miongoni mwa wanafunzi nchini.

Wanafunzi hao tayari wameshaondoka nchini kwenda Johannesburg, Afrika Kusini ambako mashindano hayo yatafanyika kati ya Agosti 13 na 20 mwaka huu.

Mashindano hayo ya yanaitwa Olimpiki ya Hisabati Afrika (PAMO). Dk. Bakari alisema taasisi yake imedhamiria kujenga nchi inayowezeshwa kidijitali.

Alitaka wanafunzi na wanazuoni wa Tanzania kupenda masomo ya sayansi, teknolojia, uandisi na hisabati (STEM), ambayo yanajenga misingi imara ya umahiri katika TEHAMA.

"Teknolojia inakua kwa kasi na hivi sasa kuna akili mnemba na programu tumizi nyingi zinazowezesha shughuli nyingi.

"Tanzania inatekeleza mpango wa kubadilisha uchumi wake kuwa wa kidijitali, ambapo TEHAMA inatumika kwenye kila sekta," alisema.

Dk. Bakari alifafanua kuwa, ushiriki wa wanafunzi na wanazuoni katika mashindano yanayoshirikisha wadau ndani ya Bara la Afrika na ulimwenguni kote una umuhimu wa kipekee.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, pamoja kuongeza stadi na kupanua weledi wa washiriki, ushiriki wa vijana hao unatangaza Tanzania na kuijengea nchi taswira nzuri kwenye majukwaa ya kimataifa.

Washiriki wa Tanzania katika mashindano ya PAMO mwaka huu na ambao wanatoka shule za sekondari ni Amborse Rutashobya wa Shule ya Sekondari ya Ufundi Iyunga; Ilham Abdalla Awadhi wa Feza, Zanzibar; Mwanaarab Said Mbwana wa Sekondari ya Lumumba, Zanzibar; Stella Maliti wa Sekondari ya Wasichana ya Marian na Zakaria Mwita wa Azania.

Mashindano ya PAMO kwa Tanzania yanaratibiwa na Chama cha Hisabati Tanzania chenye makao makuu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Mwenyekiti wa chama hicho, Dk. Said Sima, alisema wanafunzi hao watano waliibuka kidedea kwenye mashindano ya kitaifa yaliyohusisha wanafunzi 812 kutoka shule mbalimbali nchini miezi michache iliyopita.

Mlezi wa Kitivo cha Hisabati UDSM, Dk. Sylvester Rugeihyamu alisema walihangaika kutafuta wafadhili kutoka taasisi mbalimbali, zikiwamo za kiserikali na binafsi hadi TCRA ilipojitokeza.

Alishukuru mamlaka hiyo kuwaunga mkono na kufadhili wanafunzi washiriki wa mashindano hayo, akisema chama hicho peke yake kisingeweza kutuma washiriki wa Tanzania kwenye mashindano ya PAMO bila ya ufadhili wa TCRA, ambayo imetoa tiketi za kwenda Afrika Kusini na kurudi.

Aliomba taasisi nyingine kuiga mfano huo mzuri wa TCRA siku zijazo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu, wachezaji ipeni heshima mikataba yenu

**MSIMU** mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara wa mwaka 2024/2025 ulianza rasmi jana kwa mchezo mmoja uliochezwa kati ya wenyeji Pamba Jiji FC dhidi ya Maafande wa Prisons kutoka Mbeya.

Hii ni baada ya kuisubiri kwa zaidi ya miezi mitatu baada ya msimu wa 2023/2024 kumalizika.

Lakini baada ya msimu huo kumalizika, ndipo mchakato wa usajili ulianza kwa vilabu mbalimbali vinavyoshiriki Ligi Kuu na hata madaraja ya chini kuanza kusaka nyota wapya ili kuimarisha vikosi vyao.

Kwa siku za karibuni katika kipindi hicho cha dirisha la usajili kuna matukio mbalimbali yametokea yanayohusu mvutano wa usajili kuelekea msimu mpya.

Zipo timu, hususani za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo ziliwekewa pingamizi katika mchakato huo kwa sababu mbalimbali.

Tumesikia kilichotokea kwenye usajili wa Simba kwa wachezaji Lameck Lawi kutoka Coastal Union, Awesu Awesu aliyekuwa anaichezea KMC na Yusuph Kagoma.

Kimsingi viongozi wa klabu zetu na wachezaji wanapaswa kuheshimu mikataba wanayoingia ili kutoleta mvutano wakati upande mmoja unapotaka kuondoka au kuvunja mkataba huo.

Kwa bahati mbaya katika suala la usajili kwa miaka mingi sana tumekuwa tukifanya kiholela holela na ndiyo maana kumekuwa na kesi nyingi zinazohusu mikataba kwenye Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) na lile la Kimataifa (FIFA).

Inawezekana Tanzania ikawa kinara kwa kuwa na kesi za mara kwa mara zinazohusu mikataba kule FIFA, hii haipendezi na inalitia aibu soka letu. Ifike sehemu 'ujanja ujanja' uwekwe pembeni, viongozi na wachezaji wafuate taratibu kwenye kuvunja mikataba kuepuka migogoro isiyokuwa na faida kwenye soka letu.

Mchezaji anapotaka kuvunja mkataba kwenye timu moja baada ya kupata au kuahidiwa malisho mazuri kwenye timu nyingine, basi akae na uongozi wa klabu yake na wakubaliane ili aondoke kwa amani bila kuleta mvutano.

Pia kwa viongozi wa klabu, waache tamaa pale wanapoona mchezaji anakwenda kunufaika zaidi, wapo ambao wanajua kabisa kuwa mchezaji hana mkataba au umebaki chini ya miezi sita, lakini wanaweka kauzibe na hila kwenye kumruhusu mchezaji.

Hapa ndipo tunaposikia mchezaji anasema amemaliza mkataba kwenye timu yake na muda huo huo viongozi wa timu hiyo wanasema mchezaji huyo bado ana mkataba nao.

Tuache ubabaishaji kwenye masuala ya msingi, taratibu na kanuni zimewekwa ili kuepuka mvutano usiokuwa wa lazima, kila upande kwa maana ya klabu na wachezaji wanapaswa kuzifuata.

Hatutaki kurudi nyuma, tulipokuwa tunaona mchezaji akifungiwa kwa sababu ya kusaini mikataba kwenye klabu mbili kwa wakati mmoja, au klabu kutozwa faini kwa sababu ya kumsajili mchezaji mwenye mkataba na klabu nyingine, tumeshatoka huko.

Klabu kabla ya kumsajili mchezaji yeyote ijiridhishe kwanza kama kweli mchezaji huyo hana mkataba ulio hai na timu yake, hakuna sababu ya kufanya sajili za vificho, klabu zikae mezani kujadiliana, tunaamini kila timu ipo kwa ajili ya kufanya biashara kwani mpira wa sasa ni biashara.

Kwa kumalizia, kwa zile sajili ambazo Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imezitolea maamuzi kutokana na mvutano, basi klabu husika zikae meza moja na kumalizana kwa mustakabali wa soka letu pia kwa mustakabali wa wachezaji husika ambao mpira ndio kazi yao inayowasaidia kuendesha maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Kamati ya Sheria TFF isiyumbe kesi za mikataba ya wachezaji

**KWA** miaka ya hivi karibuni Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), inaonekana haifanyi kazi yake ipasavyo.

Timu zinaposhindwa kupata mwafaka na kupeleka malalamiko kwao ili kupata ufafanuzi wa kisheria na kuamua, lakini inawarudishia 'mpira' eti wakapatane wenyewe.

Wameshindwaje kupatana mwanzo na safari hii iwezekane?

Hii inashangaza kidogo, ni sawa na ugomvi wa mume na mke ambao wamegombana huko na wamekwenda kwa mtu nzima wanayeamini anaweza kuwasuluhisha na kuwapatanisha, badala yake mtu huyo anawaambia waende wakamalizane wenyewe, msuluhishi huyo anashindwa kutambua wao hawakuelewana ndiyo maana wamefika kwake.

Tumeona kesi nyingi, na hasa msimu huu ndiyo kumekuwa na matatizo hayo, tangu kesi ya Lameck Lawi kati ya Simba dhidi ya Coastal Union, pia tumeona pia kesi ya KMC na Simba dhidi ya mchezaji Awessu Awessu.

Tushukuru Mungu pamoja na yote, Simba na KMC wamekaa kama walivyoambiwa na kulimaliza suala hilo, na kwa hivi tunavyozungumza, Awessu na mali ya Simba.

Pamoja na hayo yote kunaonekana kuna matatizo kidogo katika kamati hiyo, hasa linapokuja suala la kufanya uamuzi wa kimkataba kuhusiana na wachezaji husika. Sidhani kama kuna utofauti kati ya kamati hii na ile ambayo ipo Shirikisho la Mpira wa Miguu Duniani (FIFA), ambako hatujawahi kusikia wamepelekewa kesi na wameamua kuwaridishia wenyewe waelewane.

Wao wanakwenda moja kwa moja kuangalia sheria na kanuni zinasemaje na wakaamua kulingana na jinsi walivyojiwekea, bila kujali litamuumiza mtu fulani au litamfurahisha.

Sasa unashangaa ni kwa nini Kamati ya TFF huwa haitumii sheria na kanuni zake kuamua badala yake ni kama vile inatumia busara hivi kwa kuogopa labda watu fulani watakasirika.

Sheria zipo, kanuni zipo, kwa nini hazitumii kuamua kesi za kimkataba wa wachezaji? Na kitendo chao cha mara kwa mara kuamua klabu zikaelewane wanaweza kuwa wanatengeneza mwanya kwa wachezaji wasio waaminifu, na klabu ambazo haziheshimu mikataba kurudia makosa ya aina hiyo.

Inawezekana labda ni kwa sababu kamati hiyo ina baadhi ya watu ambao si wanasheria.

Kwa maana hiyo, ipo haja sasa ya kuiangalia Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji, mbali na Mwenyekiti na Makamu wake kuwa na taaluma ya sheria, basi hata wajumbe wake wawe ni wanasheria ili waamue kutokana na sheria inavyowaelekeza na si vinginevyo.

Nikisema sheria nina maana ya sheria za mpira wa miguu, yaani wawe wamejikita kwenye sheria za mchezo huo na si za mikataba ya nyumba, magari au viwanja.

Kuna mwanasheria mmoja ameniambia mikataba ya wachezaji ambayo ipo kwenye sheria za soka, haifanani kabisa na mikataba mingine kama ya nyumba magari, viwanja, hivyo wanaotakiwa hata kuwasimamia wachezaji na klabu wawe ni watu wanaoijua.

Nadhani hata kamati nayo inatakiwa iwe na watu hao. Ndiyo maana utaona hata mchezaji akifanya makosa, siku hizi hafungiwi miezi sita au mwaka, badala yake analipishwa faini na fidia, uharaka wa kulipa ndiyo unatamfanya kuchelewa au kuwahi kuwa huru.

Kitendo cha Kamati kumrudisha Awessu katika klabu yake ya KMC binafsi naona hakikuwa sahihi kwa sababu alionekana hawezi tena kuitumikia kiasi cha kutamka kuwa yupo tayari kurejea Zanzibar kuvua samaki.

KMC nao wamekuwa waungwana, wangeweza kutumia mwanya huo kumkomoa kwa sababu wameshapewa mpini na mchezaji ameshika kwenye makali. Ndiyo maana FIFA haikubali kumrudisha mchezaji katika klabu ambayo haitaki tena. Hata kama ana kesi, wakati inaendelea inamuuliza klabu anayotaka kucheza. Huku ndiko wenzetu walipofika, lakini sisi bado tunaamua kwa 'busara' ili tusionekane wabaya.

HABARI KITAIFA

# Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru akerwa uchafuzi vyanzo vya maji

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WANANCHI wa Kijiji cha Masabi katika Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama wamesisitizwa kutunza vyanzo vya maji ili waendelee kupata huduma ya maji safi na salama.

Wito huo umetolewa juzi na kiongozi wa Mwenge wa Uhuru, Godfrey Mnzava, wakati akikagua uendelevu wa upanuzi mradi wa maji, kutoka Segese hadi Kijiji cha Masabi, kwamba chanzo chake ni kisima kirefu.

Alisema wananchi wanapaswa kuitunza miradi yote pamoja na kutunza vyanzo vya maji ili kuwa na uhakika wa maji na kuendelea kuhudumiwa kwa kupata majisafi na salama.

Alisema: "Huduma ya maji haina mbadala na kama kauli yenu ya RUWASA inavyosema 'Ruwasa maji bombani' endeleeni kusambaza maji zaidi kwa wananchi, pia kuwaunganishia majumbani mwao na kumtua mama ndoo kichwani".

Meneja Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mzingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kahama, Maduhu Magili, alisema wameutekeleza kwa mfumo wa force account, lengo likiwa ni kutatua kero ya muda mrefu ya ukosefu wa huduma ya maji safi na salama kwa wananchi wa kijiji hicho.

Alisema: "Upanuzi wa mradi huu wa maji umenufaisha wananchi wa Kijiji cha Masabi wapatao 2,400, na gharama zake ni Sh. milioni 64.6".

Baadhi ya wananchi wa kijiji hicho walisema utekelezaji wa mradi huo umewaondolea adha ya kufuata maji umbali mrefu.

# Wanolewa kutathmini matokeo TPRP-IV

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WADADISI na wasimamizi wa utafiti wa kutathmini matokeo ya awamu ya nne ya mradi wa kupunguza umaskini Tanzania (TPRP-IV), wamefundwa juu ya namna ya kufanya tathmini katika mradi huo, kuja na mkakati wa kupanga mipango ya maendeleo kwa wananchi.

Akifunga mafunzo hayo juzi, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ilemela, Ummy Wayayu, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kutoka kwa viongozi wa mitaa na vijiji wakati wa ukusanyaji wa taarifa, lililoanza Agosti 13 na kuendelea hadi Agosti 31, mwaka huu.

Wayayu alisema mradi huo unalenga kuboresha maisha ya kaya zinazokabiliwa na umaskini uliokithiri kwa kuziwezesha kuongeza kipato na uwezo wa kugharamia mahitaji yao muhimu.

Alisema tathmini hiyo ni muhimu ili kufahamu kama mradi unatoa manufaa kwa walengwa na jamii kwa ujumla.

Mkurugenzi wa Tathmini, Ufuatiliaji, Mifumo na Mawasiliano, Japhet Boaz, alisema imepata dola za Marekani milioni 50 (Sh. bilioni 135.5) kutoka Umoja wa Nchi Wazalishaji wa Mafuta Duniani (OPEC) kwa ajili ya kutekeleza mradi huo katika mikoa ya Njombe, Arusha, Mwanza, Simiyu, na Geita ikiwa ni hatua ya kuongeza huduma za jamii na kuinua uchumi wa kaya.

Meneja wa Takwimu Mkoa wa Mwanza, Goodluck Lyimo, alisema mafunzo hayo yanalenga kuwapa washiriki uwezo wa kuelewa taratibu za ukusanyaji taarifa na mbinu zinazotumika ili kupata taarifa sahihi.

Alisema: "Takwimu hizi zitatumika katika ngazi zote za utawala ili kusaidia katika kupanga mipango ya maendeleo ya wananchi na kufanya maamuzi sahihi."



Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Simon (katikati), akizungumza jambo, alipotembelea banda la kampuni ya Kunismart inayotengeneza kuni mbadala zinatokana na taka kavu za mimea, baada ya kufungua mafunzo ya matumizi ya nishati safi kupitia programu ya mapishi hodari kwa baba na mama lishe wapatao 70, iliyoandaliwa na kampuni ya INTERFINi kwa ushirikiano na Maestro Africa Solutions kwa ufadhili wa benki ya CRDB, wilayani humo, mkoani Pwani jana. Kulia ni Mwakilishi wa kampuni hiyo, Inocent Mayawa. **PICHA: MARGARET MALISA**

# NBS yataka ushirikiano utafiti viashiria vya ajira

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, amewataka Watanzania wanaofikiwa na utafiti wa viashiria vya ajira nchini kutoa ushirikiano kwa makarani ili kuisaidia serikali kufanya mipango sahihi kwa kuendana na hali za wananchi.

Alitoa rai hiyo juzi jijini Mwanza wakati akikagua maendeleo ya kazi za kitakwimu na kueleza kuwa wanatarajia kuzifikia sampuli na kaya 14,500 kupata taarifa zao juu ya hali ajira ndani ya kaya.

Alisema hatua hiyo ni kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na Sheria ya Takwimu Sura Namba 351 inayoitaka serikali kufanya mipango kwa ajili ya wananchi kupitia takwimu zinazokidhi viwango vya kimataifa.

"Pia, sheria hii inawataka wananchi kuhakikisha mnatoa takwimu sahihi kwa makarani zinazohusu shughuli zote mnazozifanya kwa muda wa saa 24 kila siku bila kujali zipo kwenye mfumo wa ajira rasmi au shughuli binafsi," alisema Dk. Chuwa.

**"Pia, sheria hii inawataka wananchi kuhakikisha mnatoa takwimu sahihi kwa makarani zinazohusu shughuli zote mnazozifanya kwa muda wa saa 24 kila siku bila kujali zipo...**

Ofisa Mkuu wa Ufuatiliaji wa Tathmini kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Dk. Aggrey Kinasha, aliiomba NBS kuhakikisha inatoa ripoti ya takwimu hizo mapema iwezekanavyo ili kuwasaidia kufanya tathmini ya matokeo ya miradi iliyopita pamoja na utekelezaji wa miradi mipya.

Alisema takwimu hizo zinakusanywa katika wilaya 10 na mikoa mitatu na kuwa itawasaidia TASAF kuandaa andiko la mradi mwingine na kutathmini utekelezaji kuendana na takwimu hizo.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala alisema wajibu wa serikali ni kuhakikisha jukumu hilo linatekelezwa kwa ukamilifu na kuwa kama viongozi wataendelea kuwahimiza wananchi kutoa takwimu sahihi katika zoezi hilo.

Diwani wa Kata ya Kiseke, Mwevi Ramadhan alisema wananchi wapo tayari na kwa maeneo ambako kazi hiyo imeanza kutekelezwa, kwamba wametoa ushirikiano wa kutosha kutokana na zoezi kuwa sehemu ya mipango ya serikali ya upatikanaji wa fursa za ajira nchini.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Vituo vya afya vyakabiliwa na tatizo huduma ya maji

**Na Beatrice Shayo**

MKURUGENZI Mkaazi wa Shirika la WaterAid, Anna Mzinga, amesema bado kuna changamoto ya upatikanaji wa maji hasa katika zahanati na vituo vya kutoa huduma za afya.

Mzinga aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa mkakati wa Shirika la WaterAid kwa kuwashirikisha wadau wa maji na usafi wa mazingira (WASH).

Alisema maeneo hayo yanawakumba wanawake wengi ambao ndio watumiaji wa vituo vya afya hasa katika mambo ambayo yanahusika na uzazi.

"Tumeona kuna vituo vya afya ambavyo vinaonesha huduma za maji na usafi wa mazingira hazijafika, hili tunaliona ni tatizo ambalo linaweza kutatuliwa kwa pamoja ndio maana tumeamua kuanzisha mpango mkakati wa kuonesha maeneo ambayo tunaweza kuyafanyia kazi ili kuwasogeza huduma za maji hasa katika vituo vya afya na shule zetu," alisema Mzinga.

Mzinga alisema wanaunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kumtua mama ndoo kichwani kwa namna wanavyoona sehemu za kutoa huduma na kufikisha maji nyumbani bado haijafikia kwa asilimia 100.

Alisema kutokana na changamoto hiyo wameona athari kubwa inaenda kwa mwanamke na kwa mtoto wa kike. Kutokuwapo kwa asilimia 100 ya maji na usafi wa mazingira inachangia kuwarudisha nyuma wanawake kiuchumi.

Aidha, alisema mpango mkakati huo waliouanzisha wamejipanga katika kuleta taarifa rasmi ni wapi kunahitajika kufanyiwa kazi.

Alisema wanawekeza zaidi kufanya utafiti na kufuatilia maeneo ambayo yanahitaji kuwekwa kipaumbele na jambo jingine ni kuunganisha wadau ili kupanga kwa pamoja katika kutekeleza mkakati huo.

Naye Mbunge wa Nzega Vijijini, Dk. Hamis Kigwangalla, aliwataka wadau wa maji na usafi wa mazingira kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa sera na mipango yake ili kuwezesha utoaji wa huduma ya maji na usafi katika jamii.

Kigwangalla ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Wabunge wanaopiga vita Usugu wa Dawa Tanzania (Uvida) alisema licha ya Tanzania kuwa na sera na mipango mizuri, hakuna utekelezaji. "Tuna wasomi wazuri ambao wamesoma na wamehitimu vizuri sana, wanaweka mipango vizuri, lakini tunakwama kwenye utekelezaji," alisema.

Alisema kupitia mkutano huo, wadau waazimie kuweka mikakati ya kufanikisha mipango iliyowekwa. "Kwanza ni kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa fedha za kutosha kwenye miradi ya maji na usafi wa mazingira kwa ujumla wake na pili ni kuhakikisha wadau wote wanakuja pamoja kusukuma ajenda hiyo ya mazingira kwa lengo la kumpa kipaumbele mwanamke," alisema.

"Tatu, tunapaswa kuielimisha jamii ili kila mmoja ashiriki. Kwa mfano unakuta kampuni kubwa za biashara (anazitaja), wananunua mazao wanafanya kazi na wananchi wanaweza kujenga vyoo kwenye zahanati wanaweza kufanya hivyo," alisema.

Mkuu wa kitengo cha sera na ushawishi kutoka WaterAid, Christina Mhando, alisema hadi mwaka 2021 vyanzo vinaonyesha kulikuwa na takribani vituo vya afya 8,549 zikiwamo zahanati 7,200 ambazo sawa na asilimia 74 zinamilikiwa na serikali.

Alisema karibu nusu ya vituo hivyo havina maji ya bomba na hata vilivyounganishwa na maji ya bomba havipati maji ya uhakika.

"Hadi asilimia 44 ya vyumba vya madaktari na asilimia 42 ya vyumba vya uzazi havina sehemu ya kunawia mikono ili kuwawezesha watoa huduma kufanya kazi kwa usafi.

Alisema hali hiyo inawaathiri watoa huduma walio mstari wa mbele kama wauguzi, wakunga na wanawake wakati wa kujifungua na wagonjwa wengine.

Naye Muuguzi na Mkunga wa kituo cha afya cha Msanga Wilaya ya Kisarawe mkoani Pwani, Robart Mgema, alisema awali walikuwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji kituoni hali iliyowalazimu kinamama kuja na maji kwenye kituo cha afya wanapotaka kutibiwa.

Alisema kwa sasa wanashukuru kupatiwa Mradi wa Maji na Shirika la WaterAid hali ambayo imewanufaisha wanawake kupata huduma sahihi katika mazingira bora.



Baadhi ya wakazi wa Dar es Salaam, wakivuka Barabara ya Morogoro, eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo jana, kwa kupita sehemu ya uzio uliobomolewa na gari, badala ya kutumia daraja maalum la juu la waenda kwa miguu, kitendo ambacho ni hatari kwa usalama. **PICHA: SABATO KASIKA**

# 5,000 watibiwa bure magonjwa ya macho

**Na Mwandishi Wetu**

ZAIDI ya wagonjwa wa macho 5,000 wamepatiwa matibabu bure, ikiwamo huduma ya upasuaji iliyotolewa na Jumuiya ya Jamii ya Khoja Shia mkoani Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utoaji wa matibabu hayo, Mwenyekiti wa jumuiya hiyo mkoani Dar es Salaam, Mohammedraza Dewji alisema ni kielelezo cha jamii ya Khoja Shia nchini kuhakikisha kila mtu anapata mafundisho ya Imam Hussain (AS).

Alisema kambi hiyo ya siku tatu ilitoa mafunzo kuhusu Imamu Hussain (AS), kujitoa kwake huko Karbala nchini Iraq katika kuokoa umma wa babu zake Mtume Mohammad (S.A.W).

"Mafunzo hayo ya Imamu Hussain (A.S), yalitaka jamii kuishi kwa haki na kufuata misingi na maadili mema bila ya kujali dini ya mtu, jinsia yake, kabila lake na hata rangi yake," alisema.

Alisema mbali na kambi hiyo kutoa elimu na mafundisho ya Imamu Hussain (AS), pia zilitolewa huduma za kibingwa za macho, uchangiaji wa damu salama, upimaji wa saratani ya shingo ya kizazi, kansa ya matiti, upimaji wa tezi dume kwa wanaume pamoja na magonjwa yasiyoambukiza.

"Huduma ya upimaji ilifanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam na tulifanikiwa kuwapima wagonjwa wapatao 5,818 na kesi za upasuaji mtoto wa jicho watu 298 walibainika na tatizo," alisema Dewji.

Kadhalika, alisema zaidi ya wananchi 2,469 walibainika na tatizo la macho na kupewa miwani, huku uniti za damu 2,816 zilikusanywa. Mkuu wa jopo la madaktari katika kambi hiyo, Dk. Amir Khanji alisema ugonjwa wa afya ya akili umesahaulika hususani katika jamii na wengine wanaufananisha na ushirikina.

Alitoa rai kwa watu wanaioshi na watu wenye msongo wa mawazo kuwa nao karibu na kuongea nao ili kubaini tatizo.

Dk. Khanji alisema upande wa maradhi yasiyoambukiza yanatokana na mfumo wa maisha wa kula vyakula vinavyozalisha sukari kwa wingi pamoja na vya mafuta kwa wingi.

Alisema pia kula mlo usiokamilika pamoja na kutokutenga muda maalumu wa kufanya mazoezi. Alishauri kwa watu hususani wafanyakazi kutumia vifaa vya kitaalamu ambavyo vitatumika kama kinga ya kutokupata maradhi wakati wa shughuli zao.

Alisema kwa watu ambao wanafanya kazi katika mazingira ya vumbi wanapaswa kuacha kufikicha macho wanapohisi yanawasha na wanaokaa ofisini kuacha kutumia kompyuta kwa muda mrefu.

# Mwenyekiti CCM aagiza kurejeshwa kazini viongozi waliosimamishwa

**Na Benny Kingson,**
TABORA

MWENYEKITI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Tabora, Said Nkumba, ameagiza kurejeshwa kazini viongozi wote wa chama waliosimamishwa kazi kwa makosa mbalimbali isipokuwa makosa ya jinai ili kuanza pamoja kujiimarisha na kuwa na mshikamano kuelekea uchaguzi ujao.

Alitoa agizo hilo kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya chama hicho mjini hapa na kuwataka wanachama wote na viongozi kuwa kitu kimoja na kujipanga kukiimarisha chama chao.

"Naagiza viongozi wote waliosimamishwa kwa makosa mbalimbali isipokuwa ya jinai warejeshwe mara moja ili tuanze upya kwa pamoja kukijenga chama, tuna chaguzi zipo mbele yetu hivyo hatuwezi kuweka mikakati ya ushindi wakati wengine wamesimamishwa, wana vinyongo, wengine walitengenezewa ajali tu," alisema.

Aliwasisitiza viongozi wa chama hicho kuacha majungu, fitina, kuhujumiana na kutengenezeana kesi zisizo na msingi badala yake wawe wamoja na wenye mshikamano ili kuwa na timu yenye nguvu katika chaguzi zijazo na hatiamaye kupata ushindi wa kishindo.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, akitoa taarifa yake katika kikao hicho alisema katika mwaka wa fedha 2023/2024, mkoa huo uliidhinisha bajeti yenye jumla ya Sh. 319,412,475,00 zikihusisha Sh. 214,545,256,00 matumizi ya kawaida.

Alisema kati ya hizo Sh. 104,867,219,00 za maendeleo na bajeti hiyo ina ongezeko la takribani asilimia 10 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2022/23 ambayo ilikuwa Sh. 219,066,021,000 na hadi kufikia Juni 30, 2024, Sh. 290,925,053,745 zilikuwa zimepokewa ikiwa ni sawa na asilimia 91 ya zilizoidhinshwa.

Alisema halmashauri zimeendelea kuongeza jitihada za kukusanya mapato na baadhi zimevuka lengo lililowekwa hadi kufikia Juni mwaka 2024 jumla ya Sh. 35,261,115,434.15 zilikuwa zimekusanywa ikiwa ni asilimia 101 ya lengo la kukusanya Sh. 35,014,984,000.



# RC abana watendaji utekelezaji wa miradi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ameagiza watendaji katika halmashauri za mkoa huo kuhakikisha wanakamilisha utekelezaji miradi yote ya maendeleo hadi kufikia mwisho mwa mwezi huu.

Alitoa agizo hilo jana wakati wa majumuisho ya ziara yake ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo katika Manispaa ya Singida.

Halima alisema kuwa miradi yote iliyoanza kutekelezwa katika kipindi cha miaka mitatu nyuma, lazima ikamilike ili wananchi waanze kupata huduma mbalimbali za kijamii kwa muda mwafaka.

"Lengo la miradi hii si kuona majengo, bali ni kutoa huduma inayotakiwa, lazima majengo yakamilike kwa wakati na katika matatizo, viongozi wakae na kutatua changamoto hiyo ili miradi isikwame," alisema.

Alisema maeneo yote ya miradi ambayo yana migogoro, lazima viongozi wakae na wahusika ili kuondoa changamoto hizo kwa wakati, nia ikiwa ni kuona wananchi wanaanza kupata huduma bora na za msingi karibu na maeneo yao.

Halima alipongeza hatua zinachukuliwa na watendaji katika kusimamia na kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo ili iweze kutekelezwa kwa viwango na ubora unaotakiwa.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alimhakikishia Mkuu wa Mkoa wa Singida kuwa miradi yote inayotekelezwa mkoani humo itakamilika kwa wakati na kwa kuzingatia thamani ya fedha iliyotolewa.

Dk. Mganga alisisitiza watendaji wote washiriki kikamilifu katika kusimamia miradi iliyoko kwenye maeneo yao ili wananchi wafurahie huduma bora zinazotolewa na serikali yao.

Mkuu wa Wilaya ya Singida, Godwin Gondwe, alisema atafanya kazi usiku na mchana kwa ushirikiano na watendaji wengine ili kuhakikisha miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa katika wilaya yake, inakamilika hadi mwishoni mwa mwezi huu kama maelekezo ya serikali yanavyotaka.

# 'Vyakula vinavyouzwa kando ya barabara si salama'

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma imeanza operesheni ya kukamata wafanyabiashara ambao wamekuwa wanafanya shughuli zao katika maeneo yasiyoruhusiwa kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009.

Sheria hiyo inakataza wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika maeneo yasiyo rasmi, ikiwamo kando ya barabara.

Ofisa Afya Usafishaji Jiji la Dodoma, John Lugendo, alisema hayo juzi jijini hapa alipokuwa anatoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusu operesheni hiyo.

"Sheria hii inakataza vyakula kuuzwa barabarani, viuzwe ndani ya soko," alisema.

Lugendo alisema wafanyabiashara hao wengi wao wakiwamo wauza mboga, matunda na vyakula na wauzaji vyombo na urembo, wanafanya shughuli zao katika maeneo yasiyo rasmi yanayotumiwa na watembea kwa miguu, magari, pikipiki, mikokoteni na bajaji.

**"Maeneo wanayofanyia biashara zao ni kando ya barabara ambako kwa asilimia 100 vyakula hivyo lazima vitakuwa na vumbi, hivyo si salama kwa walaji," alionya.**

"Maeneo wanayofanyia biashara zao ni kando ya barabara ambako kwa asilimia 100 vyakula hivyo lazima vitakuwa na vumbi, hivyo si salama kwa walaji," alionya.

Alisisitiza jiji litaendelea na operesheni hiyo pamoja na kutoa elimu na kwa wataokaidi watakamatwa na bidhaa zao kumwaga kwenye jalala kwa sababu hazifai kuliwa na binadamu.

Pia alisema jiji litachukulia hatua za kisheria, ikiwamo kulipishwa faini kuanzia Sh. 300,000 hadi Sh. milioni moja au kufikishwa mahakamani ambako adhabu ni kifungo cha miezi sita gerezani.

Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Udhibiti wa Taka Ngumu katika jiji hilo, Dickson Kimaro, alisema maeneo wanayofanyia biashara ni hatarishi kwa maisha yao pamoja na bidhaa wanazouza.




Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Joseph Fungo akizungumza katika kikao cha kufunga mwaka wa fedha 2023/2024 cha Baraza la Madiwani, jijini humo, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Matumizi ya mabilioni ya CSR kampuni za madini yazua jambo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Madini imesema utekelezaji Kanuni na Wajibu wa Wamiliki wa Leseni za Madini kwa Jamii (CSR) umekuwa na vikwazo kadhaa licha ya kampuni za madini kuchangia zaidi ya Sh. bilioni 96.6 katika utekelezaji miradi kwa miaka sita iliyopita.

Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, alitoa kauli hiyo jana jijini hapa alipofungua kikao cha maboresho ya kanuni na wajibu wa wamiliki wa leseni za madini kwa jamii za mwaka 2023.

Alisema vikwazo hivyo vinapaswa kushughulikiwa kupitia maboresho hayo ili kampuni hizo ziongeze michango yao kwa jamii.

"Tumeona kwa mwaka 2018 hadi 2023, fedha hizo Sh. bilioni 96.6 zimetumika kutekeleza miradi CSR katika halmashauri zenye shughuli za uchimbaji madini.

"Hivyo, maboresho haya ya kanuni yamelenga kuhakikisha kunakuwa na ushirikishwaji wa pamoja kati ya jamii na kampuni za madini katika utekelezaji miradi ya jamii, jambo ambalo ni muhimu kwa maendeleo endelevu ya jamii zinazozunguka migodi," alisema.

Dk. Kiruswa alisema kuwa tangu mwaka 2017, baada ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 kufanyiwa marekebisho na kuongezwa kifungu cha 105 kinachohusu wajibu wa kampuni kwa jamii, sekta ya madini ina mafanikio makubwa.

Hata hivyo, Dk. Kirushwa alisema licha ya mafanikio hayo, utekelezaji kanuni za CSR umekuwa na vikwazo vinavyotakiwa kushughulikiwa kupitia maboresho.

"Changamoto hizo ni pamoja na mipango ya miradi ya CSR kutoandaliwa kwa wakati na ile miradi iliyoandaliwa kutotekelezwa kwa wakati; kukosekana kwa miongozo ya utekelezaji mipango ya CSR ambayo kwa mujibu wa sheria, inapaswa kuandaliwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kuwashirikisha wamiliki wa leseni za madini," Dk. Kiruswa.

Alitaja vikwazo vingine ni kupishana kwa mitazamo kati ya halmashauri na wamiliki hao kuhusiana na aina ya miradi na namna ya kuitekeleza pamoja na uelewa mdogo wa masuala za CSR kwa jamii.

Kadhalika, naibu waziri huyo alisema kumekuwa na migogoro baina ya wamiliki hao na Mamlaka za Serikali za Mitaa, hali inayosababisha baadhi ya miradi ya kijamii kutokukidhi mahitaji na matarajio ya jamii zinazozunguka migodi.

Kamishna wa Madini, Dk. AbdulRahman Mwanga, alisema wizara imeona kuna umuhimu wa kupokea maoni ya maboresho ya kanuni hizo kutoka kwa wadau ili kusaidia kupunguza vikwazo vilivyoko na kuhakikisha sekta ya madini inaendelea kuleta manufaa kwa Watanzania na taifa kwa ujumla.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alimulika utekelezaji wa matakwa ya CSR kwa kampuni za madini, akibaini kuwa kwa Mkoa Songwe, kulikuwa na udanganyifu wa kutekelezwa miradi ya mabilioni ya shilingi, ilhali hakuna mradi uliokuwa umetekelezwa kupitia fedha za CSR.





# Chuo chawezeshwa kuachana na matumizi ya kuni na mkaa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHUO cha Mafunzo Zanzibar kimekabidhiwa mfumo wa miundombinu ya nishati mbadala ya kupikia ili kuachana na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa ambayo yanachangia uharibifu mkubwa wa mazingira visiwani humo.

Mfumo huo ambao ni wa gesi pamoja na majiko umetolewa na Taasisi ya Mwanamke Initiatives Foundation (MIF) kwa ajili ya kurahisisha upikaji chakula cha wafungwa katika Gereza la Kilimani Zanzibar. Mjumbe wa Bodi ya MIF, Prof. Mohamed Hafidh Khalfan, akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, alisema kuwapo nishati mbadala katika gereza hilo, kutasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

Alisema matumizi ya nishati ya kuni na mkaa yameathiri mazingira na kuongeza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema utoaji majiko hayo yanayotumia nishati safi ya gesi kwa ajili ya kupikia, utasaidia kulinda mazingira, uendelezaji miti na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.

**"Tunaahidi kutumia majiko sanifu ya gesi kwa malengo yaliyokusudiwa sambamba na kutoa ushirikiano kwa kampuni zote zinazohusika na matumizi sahihi ya gesi na nishati mbadala,"**

Kamishna wa Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Khamis Bakari Khamis, alisema mfumo huo wa gesi utawakomboa katika kulinda mazingira pamoja na afya.

Alisema awali kila siku walikuwa wanatumia kuni nyingi kwa ajili ya kupikia, ambazo ni hatari kwa taifa hasa ikizingatiwa Zanzibar ni kisiwa. "Tunaahidi kutumia majiko sanifu ya gesi kwa malengo yaliyokusudiwa sambamba na kutoa ushirikiano kwa kampuni zote zinazohusika na matumizi sahihi ya gesi na nishati mbadala," alisema.

Mkuu wa Miradi kutoka MIF, Elex Moshi, alisema lengo lao ni kuhamasisha matumizi sahihi ya nishati safi ili kupunguza kasi ya uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji wa miti.

Alisema matumizi ya nishati hiyo itakomboa wananchi kiuchumi na maendeleo kwa kutunza mazingira na Zanzibar kuwa haiba nzuri ya mazingira yenye uoto wake wa asili.

Meneja Mkuu wa kampuni ya Gesi ya ORYX, Shuweha Khamis, alisema watahakikisha matumizi ya gesi yanakuwa endelevu kwa wananchi na kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa nishati ya nishati hiyo.




Mkurugenzi Mwendeshaji wa Taasisi ya Uhandisi wa Mtandao wa Uungaji Mabomba (DACADY), David Raymond (kulia), akitoa maelezo kwa Maofisa wa Chuo cha Mafunzo cha Jeshi la Magereza Zanzibar, kuhusu utumiaji wa majiko sanifu ya nishati ya gesi kwa ajili ya kupikia, yaliyotolewa na Taasisi ya Mwanamke Initiatives (MIF) kwa jeshi hilo, Kilimani, mjini Zanzibar jana. Wengine ni Mjumbe wa Bodi ya Taasisi hiyo, Prof. Mohamed Khafidh Khaflan (wa nne kulia) na (wa tatu kulia) ni Mkuu wa Miradi wa MIF, Elex Mushi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kamati ya Bunge yataka mikakati kusimamia watu wenye ulemavu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi wa Wakuu imeitaka Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kuweka mikakati maalum katika kusimamia maendeleo ya watu wenye ulemavu.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Machano Othaman Said, aliyasema hayo baada ya kupokea taarifa za utekelezaji kazi za wizara hiyo katika kipindi cha robo ya mwaka.

Alisema ripoti hiyo bado inaonesha watu wenye ulemavu wakiachwa nyuma, hivyo wametaka wizara iwe na mikakati ambayo itawainua katika nyanja mbalimbali ikiwamo ya kiuchumi.

Machano alisema watu wenye ulemavu wana haki ya kupata stahiki zote ikiwamo mikopo ya biashara yenye masharti nafuu na elimu.

Alisema kwa kufanya hivyo kutasaidia kuinua hali zao za uchumi na kwa kiasi kikubwa kupunguza utegemezi katika familia zao.

Mjumbe wa Kamati hiyo, Haji Shaaban Waziri, alitaka kujua kinachosababisha baadhi ya vikundi vya watu wenye ulemavu kushindwa kupata mikopo inayotolewa na serikali kuwakwamua kiuchumi.

Akiwasilisha taarifa ya vikundi vya watu wenye ulemavu kwa kipindi cha robo ya nne ya mwaka, Kaimu Katibu Mtendaji Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu, Abushiri Said Khatibu, alisema baraza hilo linasimamia vikundi vya watu wenye ulemavu 94 (Unguja vikundi 60 na Pemba vikundi 34). Alisema kati ya vikundi 94, vikundi 48 vimesajiliwa na 46 havijasajiliwa, baraza likiendelea kufanya uhamasishaji wa usajili wa vikundi hivyo kwa kufanya ufuatiliaji kupitia maofisa wa watu wenye ulemavu wa ngazi ya wilaya, mkoa, taifa na watendaji wakuu wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa lengo la kuvijengea uwezo na kuvipatia taarifa za fursa zinazotolewa.

Alisema zipo faida kadhaa zinazopatikana kwa vikundi vya watu wenye ulemavu vilivyosajiliwa, zikiwamo kuwezesha upatikanaji wa fursa za mikopo zinazotolewa na serikali, kurahisisha mawasiliano baina ya vikundi na serikali pamoja na kufaidika kwa urahisi na kutambulika.

Alisema kuna ukosefu wa elimu ya uelewa wa masuala ya watu wenye ulemavu kwa wanaotoa fursa kwa watu hao zikiwamo za mikopo.

Alisema changamoto nyingine ni kutopatikana dhamana za mikopo pamoja na kukata tamaa katika mzunguko au taratibu za uchukuaji mikopo.

# Waziri ahimiza shule kutumia mfumo mpya wa ulipaji ada

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu ya Mafunzo ya Amali Zanzibar imewataka wamiliki wa shule binafsi kuchangamkia fursa za kuwapo mfumo mpya wa kidigitali wa ufuatiliaji na ulipaji ada (LIPA ADA) ambao unarahisisha mchakato huo na wanafunzi kupata elimu bila vikwazo.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Khamis Abdullah Said, alitoa rai hiyo jana alipofungua mafunzo kwa wamiliki na wakurugenzi wa shule binafsi.

Mafunzo hayo ambayo yametolewa na Kampuni ya Tizo-Zantel kwa kushirikiana na Taasisi ya Kidigitali ya ZMotion, yanahusu utumiaji mfumo huo.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha ufanisi wa mfumo huo mpya ambao unatoa fursa kwa wazazi kulipia ada kidogo kidogo kulingana na uwezo wao na kuleta mapinduzi katika ukusanyaji ada katika shule binafsi.

Alisema mfumo kuondoa usumbufu kwa wazazi na walezi ambao wanakumbana na changamoto za malipo ya ada kwa wakati.

Mkuu wa Tigo Zantel Zanzibar, Aziz Said Ali, alisema mfumo huo ni mojawapo ya ubunifu wa kiteknolojia ulio lenga kutatua changamoto zinazokumba wazazi na shule katika ulipaji ada.

Alisema malipo kupitia mfumo huo yatafanyika kupitia huduma ya TigoPesa, hivyo kurahisisha mchakato mzima wa malipo na kuokoa muda kwa wazazi wa kwenda shuleni kulipa.

Mkurugenzi wa ZMotion Said Fuwadi, alisema mfumo wa 'LIPA ADA' umesanifiwa kwa kuzingatia mahitaji ya shule binafsi na ni rahisi kutumia.Mmoja wa wamiliki wa shule binafsi, Ameri Hassan Ameri, alisema mfumo huo ni umuhimu na utasaidia wazazi na walezi ambao awali walikuwa wakikumbana na changamoto za kufanya malipo ya ada.



**PHYNA**
UKURASA 14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
UDANI TELE

JUMAMOSI AGOSTI 17, 2024



# TUOMBE MUNGU

ENDAPO ndoa ya Zari na mume wake Shakib, ikivunjika mwanamuziki Diamond Platnumz, atakuwa njia panda kutokana na kuonekana chanzo cha wawili hao kugombana.

Mpaka sasa haijafahamika kama Zarina na Shakib, wanaendelea kuishi katika nyumba moja tangu kuanza kwa sakata hilo wiki iliyopita baada ya Diamond kusafiri hadi Afrika Kusini kusherehekea siku ya kuzaliwa kwa mtoto wake Tiffah, bila kutoa taarifa.

Ujio huo wa ghafla wa Diamond, hakumfurahisha Shakib kutokana na kuamini kwamba mke wake ambaye ana watoto wawili na Diamond, wana hisia za kimapenzi.

Kutokana na hisia hizo, Shakib ameonekana kususa na kuibua maneno makali kutoka kwa Zari na meneja wake, wakimuita mwanaume muoga na asiyejiamini.

Baadhi ya watu wanaofuatilia maisha ya mastaa, wamesema maneno makali yanayotolewa na Zari na timu yake yanaiweka ndoa hiyo katika hatari ya kuvunjika kabisa.

Saidi Komba, ameeleza kitendo cha Diamond kwenda kwa Zari bila taarifa, ni kosa kwani hata kama wawili hao wana watoto, walitakiwa kuheshimu ndoa iliyokuwapo.


"Diamond alitakiwa kutambua kuwa pale kuna maisha mengine, lazima atoe taarifa kwa mwanaume anayeiongoza nyumba kwa sasa. Shakib ana haki ya kulalamika, lakini kumtolea maneno makali sio dawa ya kumziba mdomo," amesema Komba.

Alimtaka Zari kurudi nyuma na kuangalia upya kiapo chake cha ndoa.

"Zari naamini anampenda Diamond ndio maana hataki kuwekewa mipaka, lakini anatakiwa kutafakari yeye ni mke halali anatakiwa kuishi kwa mipaka," ameongeza.

BASI SAWA

## Akothee afurahia kurudi kwenye ndoa



MSANII wa muziki kutoka Kenya, Esther Akoth, maarufu kama Akothee amesema yeye na meneja wake Nells Oaks, wamerudi upya kama mke na mume.

Akizungumzia safari yao ya nchini Uganda, Akothee amefichua kuwa huko walitumia muda wao kula kiapo cha kurudi katika maisha ya ndoa.

"Uganda tulienda kama meneja na msanii, tunarudi nyumbani kama mke na mume. Je, uliona viapo vyetu vikifanywa upya Uganda? Asanteh sana umeimarisha maisha yangu ya upendo." Ameandika katika ukurasa wake wa Instagram.

## Treyzah akubali uandishi unalipa



MSANII wa Bongo Fleva, Treyzah, amesema pamoja na kufanikiwa katika uimbaji, lakini pesa nyingi anapata kwa kuwaandikia mashairi wasanii wengine.

Amesema amekuwa katika tasnia hiyo kwa miaka mingi, lakini anaamini kazi ya uandishi ndiyo inayompa kipato kikubwa kutokana na wanamuziki wengi kuhitaji huduma yake.

"Muziki unanilipa sana katika uandishi kuliko kwenye shoo au majukwaa ya muziki. Kupitia maandishi napata pesa nyingi na hilo linanipa faraja," amesema Treyzah.



# HAMISA SASA MWENDO WA MIKOGO

MWANAMUZIKI na mwanamitindo, Hamisa Mobetto, amewakoga watu kwamba mapenzi anayoyapata anajiona tayari amefika peponi.

Mobetto ambaye yuko katika uhusiano wa kimapenzi na mwanasoka Aziz Ki, ameandika kwenye ukurasa wake wa Instagram kwamba wakati mwingine anajihisi katika hali hiyo ya furaha kutokana na mapenzi anayoyapata.

"Na kama moyo unapopenda, unajiona kama uko peponi kwa furaha," ameandika.



# Harmonize ashauriwa mazito

WADAU wa muziki wa Bongo Fleva, wamemshauri Harmonize, kujitathmini kutokana na mfululizo wa matukio ya kuachana na wanawake ndani ya kipindi kifupi.

Hivi karibuni, Harmonize na mpenzi wake Posh Queen, walitangaza kuachana na kila mmoja alitangaza kufuata njia yake tofauti.

Katika mitandao ya kijamii, baadhi ya wafuasi wa mwanamuziki huyo walimpa ushauri wa kutulia na kujitathmini kabla ya kuamua kumtafuta mwanamke mwingine ili angalau aishi naye kwa muda mrefu.

FILAMU

# Rossa: Shikamoo mapenzi




**Na Adam Fungamwango**

MSONDO Ngoma waliwahi kuimba wimbo mmoja uitwao 'penye penzi hapakosi tezi.' Wakiwa na maana kuwa siku zote kwenye mapenzi, hapakosi watu ambao watayatoa kasoro na kutaka kufanya figisu zozote zile ili wapendanao wafarakane na kuachana.

Leo tuiangalia filamu iitwayo 'Rossa'. Imechezwa na wasanii Said Lukamba, Vanesa Widambe, Mzee Makwati, Upendo Jaspa, Jenifa Salum, Mwanaidi Dihomi na wengineo.

Ni filamu inayoonyesha mtawala wa himaya moja ya Chiwale, ambaye ni mwanamke alipohangaika kupigania penzi la binti yale Dora.

Ni kwamba binti yake alimpenda kijana mmoja aitwaye Lwigila. Binti mfalme akafa akaoza, lakini kijana huyo penzi lake lilikuwa kwa binti mwingie Rossa. Huyu ni binti wa kawaida tu kwenye himaya hiyo. Mtawala aliitisha mkutano wa vijana wote nyumbani kwake ili binti yake Dora achague mchumba. Walikuja na Dora alipita kwenye mstari kuchagua, lakini Lwigila hakuwepo. Huyo ndiye alitaka kumchagua. Hali ikawa mbaya. Walipoondoka Dora alimlilia mama yake, Mtawala akaanza kutumia nguvu kutaka kulazimisha.

Kwanza akaenda nyumbani kwa kina Lwigila na kupiga mkwara wa nguvu. Akaenda nyumbani kwa msichana Rossa na kudai uchumba wa Lwigila na Rossa yeye kama mtawala hautambui.

Baada ya mkwara wa utawala wake kushindwa, sasa akaanza kutumia ndumba.

Rossa akafanywa ndodocha na Lwigila akawa mwendawazimu. Msukule wa Rossa ukatoka ulikowekwa na kukimbilia kusikojulikana. Huko ulikutana na kijana mmoja ambaye alimchukua na kumpeleka kwa mganga, akapona. Akarudi Rossa yule yule. Kijana akaamua kumrudisha nyumbani kwao.

Huku nako Lwigila aliponyeshwa kwa masharti ya kumuoa binti wa mtawala ili awe mfalme.

Wakati wakiwa kwenye sherehe ya Lwigila na binti mtawala, ghafla anamuona Rossa akiwa ameongozana na kijana mmoja. Lugwila na Rossa walionana. Kila mmoja kwenye hadhara alimuacha aliyekuwa naye na kukimbiliana. Wakakumbatiana.

# MANDOJO TUTAONANA BAADAYE

**Na Adam Fungamwango**

HAIKUWA wiki nzuri na mashabiki wa muziki za kizazi kipya hasa wagumu wa hip hop, baada ya kupata taarifa za kifo cha msanii mkongwe, Joseph Francis, maarufu kimuziki kama Mandojo.

Msanii huyo alifariki dunia Jumapili iliyopita jijini Dodoma kwa kile kilichoelezwa kushambuliwa na watu waliodhaniwa kuwa ni mwizi.

Msanii huyo alifariki njiani akiwa anakimbizwa hospitali, amezikwa Kaloleni mkoani Singida.

Wengi waliokuwa mashabiki wa muziki wakati bongo fleva inaanza mwanzoni mwa miaka ya 2000, wanamkumbuka kwa ngoma nyingi alizotoa, akiwa na pacha wake kwenye masuala ya muziki, Domokaya.

Imeelezwa kuwa msani huyo amefariki ikiwa ni siku chake tu, kabla ya kuadhimisha siku yake ya kuzaliwa, Agosti 22.

Mandojo amefariki, lakini kazi zake alizoziacha hazitofutika kamwe. Nazo ni nyimbo alizoziacha duniani ambazo zitaendelea kusikikiza milele na milele.

**Niaje**

Ni moja kati ya ngoma ambazo ziliwapa jina sana Mandojo na mwenzake Domokaya. Ilitoka mwaka 2004, wakishirikisha mkongwe Juma Nature. Maudhui ya wimbo huu wanawasema watu wenye roho mbaya, ambayo wapo tayari mwenzao aharibikiwe.

**Dingi**

Ngoma hii iliyotoka 2007, ambapo Mandojo na Domokaya walikuwa wakielezea madhila wanayoyapata watoto wanaotelekezwa na baba zao.

Msanii huyo na mwenzake walivaa uhusika na watoto hao ambao walikuwa wakimweleza baba yao jinsi alivyokuwa wakiwatesa wakati wamepata pesa.

**Nihukumu Mola**

Moja ya ngoma ambazo ukiisikia unaweza kudhani labda alikuwa akitabiri kifo chake, na hasa pale anaposema binadamu watu wanauawa wao kwa wao.

Inawezekana ikawa wakati yupo hai ukauchukulia poa, lakini hebu kausikilize sasa unaweza kukutoa machozi.

**Wanok Nok**

Kama hukumfahamu Mandojo kwa ngoma zilizotangulia, basi uanweza kumfahamu kwa ngoma hii. Ilikuwa ni moja kati ya nyimbo maarufu sana miaka hiyo, ambayo walimshirikisha msanii, Lady Jaydee, 2004.

"Wanafki nafki watu wa kupakazia, yasiyowahusu wao kuingilia, maneno yao ni kama ya simba, ukiyasikiliza lazima utayaaminia, mademu wa watu wanawarukia, kumbe ni uongo wao wenyewe ndiyo wanaowatokea..." Ni baadhi ya maneno yaliyo katika ngoma hii maarufu iliyowafanya, Mandojo na wenzake wawe wasanii wakubwa nchini.

**Nikupe Nini?**

"Nikupe nini hani, nikupe nini uridhike." Ni maneno yaliyomo katika wimbo huo ambao nao ni moja kati ya ngoma zilizompa umaarufu sana marehemu Mandojo.





# May Edochie kuburudisha Nollywood

MAY Yul-Edochie, ambaye ni mke wa zamani wa mwigizaji Yul Edochie, ameelezea furaha yake kwa kutumbuiza kwa mara ya kwanza Nollywood katika uzinduzi wa filamu mpya inayoitwa Wives On Strike 3.

Mwigizaji maarufu wa Nollywood Omoni Oboli, alichapisha trela ya filamu yake kwenye ukurasa wake wa Instagram, kisha May alichangia kwa kueleza furaha yake baada ya kualikwa kutumbuiza.

"Hatimaye nimehusika katika filamu na nimefurahi kuwepo na lazima niitazame kwa sababu imepakiwa." Aliandika May.



## Phyna uvumilivu dawa

MSHIRIKI wa Shindano la Big Brother Nigeria msimu wa saba, Phyna amechafua hali ya hewa katika mtandao wa x, akiwaita wafuasi wake kama watu wasiofaa na wanaopenda umbeya.

Kauli hiyo ameitoa wakati bifu lake na mshiriki mwingine wa shindano hilo, Wanni likipamba moto huku wafuasi wake wakionekna kuwa upande wa mpinzani wake ambaye anasema Phina sio mrembo kama anavyojiona.

Akijibu maoni ya wafuasi wake, Phyna aliwaambia kwamba akitakiwa kupima pesa na wao hatawaona kwa sababu anawaona wajinga kwa kuwa hawana uwezo wa kumwokoa.

## Sikieni ushauri wa Tems

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Tems, amesema kwamba wanamuziki wa kike hawapendani na wanakoseshana amani tofauti na wanaume.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, mwimbaji huyo amewataka wasanii hao kuiga wanamuziki wa kiume ambao kila wakati wanasaidiana.

"Nimesema hapo awali na nitasema tena, wanamuziki wa kike wanachosha sana, inachosha sana! Niambie ni kwa nini Tems na Ayra Starr hawakai pamoja kwa kujiona," ameandika.





## Dr Dre ageukia kurusha mishale

RAPA na mtayarishaji wa muziki kutoka Marekani, Dr Dre ameweka wazi dhamira yake kuwa anafikiria kugeukia michezo ili kuwania medali katika Olimpiki ya 2028.

Akizungumza katika mahojiano na Entertainment Tonight, Dr Dre mwenye miaka 59, alisema mchezo aliouchagua na anataka kushiriki Olimpiki itakayoandaliwa Los Angeles ni ulengaji mishale.

Rapa huyo amesema kwamba anatarajia kushinda medali ya dhahabu katika michezo hiyo itakayofanyika katika jimbo alikozaliwa.

## Lizzy hawezi kuiba dhahabu

MWIGIZAJI maarufu kutoka Nollywood, Lizzy Anjorin, ameeleza tuhuma anazopewa kwamba aliiba dhahabu zinamnyima furaha.

Amesema madai hayo yaliyoibuliwa Februari mwaka huu, hayafanani na yeye alivyo kwa sababu hawezi kuiba kitu kidogo kama dhahabu ya gramu 15,000.

"Hebu kwanza tuthibitishe ukweli kwamba tunazungumza juu ya dhahabu 150,000. Ni chini ya punje ya mchele kwa hivyo unawezaje kuingia sokoni na kuiba kitu kidogo kuliko punje ya mchele," amesema Lizzy.





# Vifo vya wajawazito na watoto vyapungua Arusha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SERIKALI mkoani Arusha imesema kwa kipindi cha mwaka 2023/24 kupitia programu ya M-mama imefanikiwa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto kutoka 67 hadi kufikia 48.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mganga Mkuu Mkoa wa Arusha, Dk. Edna Chonge, wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha mwaka cha tathmini ya utekelezaji wa mfumo wa huduma ya M - mama mkoani hapa.

Alisema kwa mujibu wa takwimu hizo, vifo vilivyopungua ni 19 sawa na asilimia 28.3, hatua hiyo imetokana na progamu ya M-mama inayotoa usafiri wa dharura na rufaa kwa wajawazito na watoto mkoani Arusha.

Edna alisema kwa kipindi cha mwaka mmoja na miezi mitatu ya programu hiyo imefanya mageuzi ya kupunguza vifo vya wajawazito na watoto.

Alisema katika Mkoa wa Arusha mfumo wa program hiyo ulifunguliwa Desemba 19 mwaka 2022 na kuanza utekelezaji Machi mwaka 2023, hivyo kwa kipindi hicho, mkoa huo umefanikiwa kupunguza vifo vya wajawazito na watoto kwa asilimia 28.3.

**"Kupitia programu ya M-mama tumefanikiwa kusafirisha wajawazito na wazazi 4,189 sawa na asilimia 82,watoto wachanga 808 sawa na asilimia 18 na kufikia jumla ya rufaa...**

"Kupitia programu ya M-mama tumefanikiwa kusafirisha wajawazito na wazazi 4,189 sawa na asilimia 82,watoto wachanga 808 sawa na asilimia 18 na kufikia jumla ya rufaa zilizoingizwa kwenye mfumo kuwa 4,997 sawa na asilimia 92," alisema.

Hata hivyo alisema lengo la kikao kazi hicho ilikuwa ni kufanya tathmini ya utekelezaji wa mfumo huo ili kutambua changamoto halisi na kuzitafutia ufumbuzi wa haraka.

Pia alisema baada ya kufanya tathimini walipaswa kuweka mpango mkakati wa utatuzi endelevu wa changamoto zilizojitokeza, ili kuendelea na mchakato wa kupunguza au kuondoa vifo visivyo vya lazima.

Alisema: "Lengo la kufanyika kwa kikao cha tathimini ya utekelezaji wa mfumo na utambuzi wa changamoto zilizojitokeza na kuzitafutia ufumbuzi pamoja na kuweka mpango mkakati wa kuondoa vifo au kupunguza".



Diwani wa kata ya Oljoro namba tano, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Loishiye Lesakwi (kushoto) akipokea mabomba ya maji kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kwa ajili ya kusambazwa kwenye mradi wenye thamani ya Sh. milioni 383 utakaonufaisha vijiji viwili, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Bil.2.8/- kuhudumia miradi ya maji

**Na Allan Isack,** MONDULI

SERIKALI imesema kwa kipindi cha mwaka 2024/2025 imetoa Sh.bilioni 2.8 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 11 ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli mkoani Arusha.

Miradi hiyo itatekelezwa katika vijiji 13 wilayani humo kwa lengo la kupunguza au kumaliza kabisa tatizo la upungufu wa huduma za maji kwenye vijiji vyote 62 katika eneo hilo.

Hayo yalisemwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Festo Kiswaga, wakati akifungua mkutano mkuu wa pili wa Vyombo vya Watumiaji wa Huduma za Maji ngazi ya Jamii(CBWSOs).

Alisema hadi sasa vijiji 45 vimefikiwa na huduma ya maji safi na salama kwa wastani wa asilimia 69 vikiwa vimefikiwa na huduma hiyo.

Kiswaga alisema kukamilika kwa miradi hiyo itafikisha asilimia 86 ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Wilaya ya Monduli na kupunguza tatizo hilo kwa wananchi wa eneo hilo.

Vilevile, alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wanawapatia wananchi huduma ya maji safi na salama na wananchi wana wajibu wa kulinda miundombinu pamoja na kulipa ankara za maji ili waendelee kupata huduma.

Naye Meneja wa Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Wilaya ya Monduli, Neville Msaki, alisema hali ya mwendeno wa uendeshaji wa skimu za maji unaendelea vizuri. Kadhalika alisema upande wa vyombo vya watumia maji baadhi ya viongozi wamekuwa changamoto, huku jumla ya vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii 20 vilivyoudwa vilisajiliwa kwa mujibu wa Sheria Na.5 ya Mwaka 2019.

Aidha alisema hadi sasa vyombo hivyo 10 vinaendelea kutekeleza majukumu kama inavyotakiwa kwenye maeneo yao ya ni Mtowambu, Lolkisale, Makuyuni, Naitolia, Mswakini Juu, Naiti, Meserani Bwawani, Selela, Mbaashi na Saruni Oldonyo.

Pia alisema kuna vyombo sita vinafanya kazi kwa kusuasua ambavyo ni Monalo, Mfereji, Enguik, Lendikinya, Emairete, Eluwai na Lemoot.

Katika hatua nyingine, alisema kuna vyombo viwili havijanza kufanya kazi ambavyo ni Mswakini Chini na Engaruka, pia wameanzisha vyombo viwili vipya ambavyo ni Lepuruko na Nafco.

# DC: Lishe kwa watoto Ngorongoro imeimarika

**Na Allan Isack,** NGORONGORO

MKUU wa Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, Kanali Wilson Sakulo, amesema kutokana na tathimini iliyofanyika hivi karibu hali ya lishe kwa watoto wilayani humo imeendelea kuimarika ukilinganisha na ilivyokuwa awali.

Alisema hayo juzi wakati wa kikao cha tathimini ya utekelezaji wa shughuli za lishe kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Julai mwaka huu.

"Hali ya lishe kwa watoto kwenye wilaya yetu imeendelea kuimarika kutokana na kuongezeka kwa asilimia za hali nzuri ya lishe kwa kuwa zimepanda ukilinganisha na vipindi vilivyopita," alisema.

Kadhalika, alitoa rai kwa watendaji wa kata kuendelea kusimamia vyema shughuli za lishe katika kata zao, ili kuhakikisha wilaya hiyo inaendelea kuwa na watoto wenye hali nzuri ya lishe.

"Licha ya kuwa tuna viashiria vizuri vya hali ya lishe, sitapenda kuona watu wanalipana posho halafu hakuna kinachofanyika, hivyo natoa rai kwa watendaji wa kata kasimamieni vizuri shughuli za utekelezaji wa masuala ya lishe kwenye kata zenu," alisema Kanali Sakulo.

Pia aliwataka watendaji hao kuwa na ushirikiano wenye tija na vikundi vya wanawake vilivyopo katika kata zao ili kujenga jamii yenye upendo.

"Ikumbukwe kuwa Halmashauri ya Ngorongoro kupitia wataalamu na uwezeshaji kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, ilifanya zoezi la utoaji wa matone ya vitamin A na dawa za minyoo katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kliniki za mkoba ambapo jumla ya watoto 51,115 kati ya 54,898 walifikiwa," alisema.

Ofisa Lishe wa Wilaya ya Ngorongoro, Angela Mbaga, akisoma taarifa ya utekelezaji wa shughuli za lishe kwa kipindi hicho alisema watoto 35,503 walifanyiwa tathmini ya hali ya lishe.

Alisema idadi ya watoto 33,004 sawa na asilimia 92.96 walikutwa na hali nzuri ya lishe na asilimia 6.79 sawa na watoto 2, 410 walikutwa na hali ya hafifu ya lishe. Aidha, alisema kwa kipindi cha miezi mitatu walifanya maadhimisho ya siku ya afya na lishe katika kata nane ikiwemo Oloipiri, Endulen, Samunge, Kirangi, Orgosorock, Olorien, Enguserosambu na Maalon.

Vilevile alisema katika maadhimisho hayo yalihusisha utoaji wa huduma za kliniki ya mkoba, upimaji wa hali ya lishe kwa watu wazima na kutoa ushauri nasaha kuhusu lishe bora.

Alisema wajawazito 5, 940 walipatiwa elimu ya lishe ya makundi ya chakula, uandaaji wa mlo kamili na chakula cha nyongeza kwa watoto.

Pia, alisema walitoa vidonge vya madini chuma kwa wajawazito ili kuendelea kuboresha hali ya afya timamu kwa wajawazito.

Alisema: "Tukiwa kama watendaji wa serikali tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi ili kuhakikisha suala la lishe katika halmashauri yetu linaimarika zaidi ili kuwapo kwa hali nzuri ya lishe".

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Tukuyu, MECCO zilivyozitikisa Simba, Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KWA miaka mingi sasa mkoa wa Mbeya umekuwa ukitoa timu tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Siyo kama mikoa mingine haijawahi kutoa, lakini mkoa huo umeendelea kutoa vikosi vya timu ambazo hata kama hazijachukua ubingwa, lakini zimekuwa imara na kuogofya si kwa timu zinazocheza Ligi Kuu tu, lakini hata kwa timu kongwe zinazopishana kutwaa ubingwa, Simba na Yanga.

Miaka michache iliyopita ilitoa timu tishio kama Mbeya City baadaye ikashuka daraja, Mbeya Kwanza ambayo nayo imeshuka na Ihefu, iliyogeuzwa kuwa Singida Black Stars.

Pamoja na hayo kuna timu za Prisons iliyo Ligi Kuu kwa muda mrefu na KenGold iliyopanda daraja msimu huu.

Ni nadra sana kwa Ligi Kuu Tanzania Bara kuchezwa bila ya kuwa na timu kutoka Mbeya, kama ilivyo kwa Dar es Salaam. Kuna wakati ligi ilichezwa bila ya kuwa na timu kutoka Morogoro, Tanga, au Mwanza, mikoa ambayo inajitahidi sana kutoa timu za Ligi Kuu.

Mkoa wa Mbeya unafanana na mkoa wa Dar es Salaam kwa kuwa na timu za Ligi Kuu. Mfano msimu huu Dar ina timu za Simba, Yanga na Azam, Mbeya wakiwa na Mbeya City, Mbeya Kwanza na Prisons, ingawa kwa sasa maafande hao wanatumia Uwanja wa Nelson Mandela kwenye mechi zao za Ligi Kuu, ili tu kuepusha msongamano.

Tunakumbuka kuwa Mbeya City ilipopanda Ligi Kuu ilivyokuwa ni timu ya namna gani.

Tunakumbuka msimu wa 2013/14 ilipopanda Ligi Kuu, ikavihenyesha vigogo vya soka nchini, Simba, Yanga na Azam, kiasi kwamba haikushangaza iliposhika nafasi ya tatu msimu huu, na msimu uliofuata ikashika nafasi ya nne.

Ndiyo timu iliyokuwa na mashabiki wengi ukiondoa Simba na Yanga, mitaani wakivaa jezi zao na mashabiki wao wakisafiri popote pale timu yao inapokwenda kucheza.

Prisons sina haja ya kuielezea. Pamoja na kwamba yenyewe inacheza tu ili ibaki Ligi Kuu, lakini imekuwa ikizipa mechi ngumu Simba na Yanga, pia kuwahi kuchukua ubingwa wa Jamhuri ya Muungano mwaka 1999 na kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Klabu Bingwa Afrika.

Sasa kabla ya timu hizo, huko nyuma kuna timu za Tukuyu Stars na Mecco zote za Mbeya, zilifanya maajabu ambayo hadi leo yanaendelea kukumbukwa, na kuandikwa kwenye historia ya soka, ili isomwe na vizazi vyote vijavyo. Ni historia ambayo inaendelea kuupaisha mkoa wa Mbeya hadi leo.



Kikosi cha Tukuyu Stars ya Mbeya kilichotwaa ubingwa wa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara 1986, sasa Ligi Kuu ya Tanzania Bara.



Kikosi cha Mecco kilichotikisa mwishoni mwa miaka ya 1980 na 1990 mwanzoni, kiasi cha timu kongwe za Simba na Yanga kudhani kuwa wachezaji wake wanatumia dawa za kuongeza nguvu.

Mwaka 1886, timu ya Tukuyu Stars ya Mbeya, ilipanda daraja na moja kwa moja ikaenda kutwaa ubingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ikawa ni rekodi ya aina yake ya timu kupanda na kuchua ubingwa. Jambo hili liliziumiza timu za Simba na Yanga. Kama kawaida yao, walichofanya ni kuisambaratisha.

Wanagawana wachezaji wa timu hiyo, wengi walichukuliwa na Yanga, wengine wakaelekea Simba.

Zilifanya hivyo kwanza ili kupata wachezaji wazuri, kwa sababu Tukuyu ilionekana kuwa na wachezaji wenye uwezo mkubwa. Pili ni kuinyong'onyesha timu hiyo, kwani wangeiachia, ingeweza kuchukua tena mara ya pili. Ikichotokea ni kwamba Tukuyu ikashika daraja baada ya wachezaji wake wengi mastaa kuchukuliwa.

Baadhi ya wachezaji wa Tukuyu Stars waliowika ni Mbwana Makata ambaye kwa sasa ni kocha wa Dodoma Jiji, aliyekuwa golikipa, Ally Kimwaga, Michael Kidilu, baadaye akaenda Simba, Godwin Aswile aliyechukuliwa na Yanga, baadaye kujiunga na Simba, Selemani Mathew Luongo, alijiunga na Yanga, baadaye naye akaenda Simba, Aston Pardon, aliyemalizia soka lake Simba, Salum Kabunda aliyekwenda Yanga, Justin Mketeke naye alikwenda Yanga, Karabi Mrisho, Richard Lumumba, Peter Mwakibibi na Kelvin Haule ambaye naye alikwenda kujiunga na Simba.

Wengine ni John Alex aliyekwenda Yanga na Yusuph Kamba. Hiki kilikuwa kikosi cha dhahabu cha Tukuyu Stars.

Baada ya kufanyiwa figisu na kushuka daraja, ikaja timu nyingine ya Mbeya, inaitwa Mecco. Ilikuwa inamilikiwa na Kampuni ya Ujenzi ya MECCO.

Ilikuwa ni balaa. Haikuchukua ubingwa, lakini ilikuwa timu tishio kiasi cha klabu za Simba na Yanga kuogopa hata kucheza nayo. Waliituhumu kuwa wachezaji wao wanatumia madawa ya kuongeza nguvu kutokana na stamina, kasi na kutochoka kwa dakika zote 90. Ilisemekana ilikuwa na uwezo wa kucheza hata dakika 200 bila kuchoka. Ilikuwa ni mtihani mzito kucheza na timu hiyo, ambayo inasemekana ni mazoezi ya milimani, hali ya hewa ya Mbeya na aina ya vyakula, ndivyo vilivyokuwa vikifanya wachezaji wa timu hiyo kuwa hivyo. Na hata walipopimwa ilionekana hawatumii dawa.

Nayo ilitamba kuanzia mwaka 1990. Baadhi ya wachezaji wake wasiosahaulika ni George Mangula aliyekuwa langoni, Rashid Mandanje, Gabriel Mwitika, Mbaga Mwantiku, Charles Makwaza, mkoba na nahodha wa timu, Danford Ngessi, Abel Kasabalala, John Kanyiki, Betwel Afrika, Ephraim Kayeta na Nassib Abass. Wachezaji wa akiba walikuwa ni Juma Hamadi, Jaffar Nyoni, Idd Mzomwe na Augutine Sanga.

HABARI KIMATAIFA

# Russia yaituhumu NATO kuisaidia Ukraine

**MOSCOW,** RUSSIA

MSAIDIZI wa karibu wa Rais wa Russia, Vladimir Putin, amesema uvamizi wa wanajeshi wa Ukraine ndani ya Russia umepangwa Nato.

Nikolai Patrushev, alinukuliwa na gazeti la Russia la Izvestia, akisema Jumuiya ya kujihami ya Nato na nchi za Ulaya, zilihusika katika kupanga uvamizi unaoendelea wa wanajeshi wa Ukraine katika eneo la Kursk.

"Operesheni katika eneo la Kursk pia ilipangwa kwa ushirikiano wa Nato na huduma maalum za nchi za Magharibi," gazeti la Izvestia limemnukuu Patrushev.

"Taarifa za uongozi wa Marekani kwamba haikuhusika katika uhalifu uliofanywa na Ukraine katika eneo la Kursk si za kweli, bila ushiriki wao na usaidizi wa moja kwa moja, Ukraine isingeingia katika eneo la Russia." Alisema.

Mapema wiki hii, Ikulu ya Marekani ilisema kwamba haikuwa na taarifa ya Ukraine kuingia Russia.

Wakati huo huo, vikosi vya Ukraine vinaendelea kusonga mbele katika pande mbalimbali ndani ya nchi hiyo.

Katika hali isiyo ya kawaida, nchi hiyo imeanzisha ofisi ya kijeshi ndani ya Russia.

Taarifa kutoka katika jeshi la Ukraine, inaeleza imefungua ofisi ya utawala wa kijeshi katika eneo la Kursk magharibi mwa Urussia baada ya kufanya uvamizi wa kushtukiza.

Kulingana na kamanda mkuu wa kijeshi, Jenerali Oleksandr Syrsky, alisema ofisi hiyo itadumisha sheria, utulivu na kukidhi mahitaji ya haraka ya watu katika eneo hilo.

Katika video iliyowekwa kwenye mitandao ya kijamii jana, Jenerali Syrsky alionekana akiuambia mkutano ulioongozwa na Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, kwamba ofisi hiyo imeanzishwa kwenye maeneo yanayodhibitiwa na Ukraine.

Wakati huo huo, Waziri wa Ulinzi wa Russia Andrei Belousov, alisema nchi yake itatuma wanajeshi zaidi kwa ajili ya kulinda watu katika eneo hilo.

Jenerali Syrsky, kuwa wanajeshi wa Ukraine walikuwa kilomita 35 ndani ya eneo la Kursk, ambapo wanadhibiti eneo la kilomita za mraba 1,150, pamoja na makazi 82.

Uvamizi huo uliofanyika siku 10 zilizopita umeelezwa ni mkubwa zaidi wa kufanywa na Ukraine ndani ya Russia tangu kuanza kwa vita mnamo 2022.

Hata hivyo, Ukraine ilisema haina nia ya kuchukua eneo la Russia.

Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Ukraine, Heorhiy Tykhy, alisema uvamizi huo ni jaribio la kuishinikiza Russia kukubali kurejesha amani ya haki.

**BBC**




Wakazi wa Gaza wakielekea maeneo salama kutokana na mashambulizi ya Israel yanayofanywa kila siku. **PICHA: REUTERS**

# Jeshi Sudan lakubali mazungumzo ya amani

**GENEVA,** USWIS

UJUMBE wa jeshi la Sudan unatarajiwa kuwasili nchini Uswis kujiunga na mazungumzo ya amani yanayoongozwa na nchi za Marekani, Saudi Arabia na Uswisi. Hapo awali jeshi lilisusia mazungumzo hayo ya kusitisha mapigano.

Hatua hii inakuja baada ya shirika la habari la Sudan SUNA, kuripoti kuwa mtawala wa kijeshi wa Sudan, Luteni Jenerali Abdel Fattah al-Burhan alikubali kushiriki mazungumzo hayo kwa sharti kwamba yaongozwe na wapatanishi wa mkutano wa awali uliofanyika Jeddah nchini Saudia Arabia mwaka uliopita.

SUNA ilimeripoti kuwa Burhan, ambaye ni mwenyekiti wa Baraza Tawala la Sudan alieleza hakuna kipingamizi kukaa na wapatanishi hao ili kujadili nao namna ya kutekeleza usitishaji mapigano.

Mnamo Agosti 14, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alifanya mazungumzo kwa njia ya simu na Burhan na kumhimiza kutuma ujumbe wa jeshi kwenye mazungumzo hayo.

Shirika binafsi la Tovuti ya El Balad News liliripoti jana likinukuu vyanzo vya serikali kuwa ujumbe wa jeshi ulitarajiwa kuwasili Geneva jana. Jeshi lilisusia mazungumzo ya Geneva na mahasimu wao kutoka kundi la wanamgambo wa RSF na wadau wengine wa Sudan, ambayo yalianza Agosti 14, mwaka huu baada ya kutoa masharti kadhaa ya kushiriki mazungumzo hayo.

Hapo jana mjumbe wa Marekani anayeongoza majadiliano hayo, Tom Perriello, aliarifu kuwa jeshi la Sudan bado lilijitenga na mazungumzo, lakini akaongeza kwamba walikuwa wanaendelea kuwa na mawasiliano nalo kila siku, na kupiga hatua kuhusu usambazaji wa msaada wa kibinadamu.

"Ukweli ni kwamba, katika siku na zama hizi, kila mmoja katika muungano huu wa kidiplomasia naweza kuzungumza na uongozi wa Jeshi la Sudan na RSF kila siku," Alisema mjumbe huyo wa Marekani kwa Sudan.

**DW**

# Rais wa Palestina atangaza kwenda Ukanda wa Gaza

**ANKARA,** UTURUKI

RAIS wa Mamlaka ya Ndani ya Palestina, Mahmood Abbas, ametangaza uamuzi wake wa kwenda Ukanda wa Gaza pamoja na viongozi wengine wa Palestina.

Akizungumza katika Bunge la Uturuki, Abbas alisema hata kama maisha yake yatakuwa hatarini atakwenda katika eneo hilo ambalo Wapalestina wanateseka.

"Nimeamua kwenda Gaza pamoja na viongozi wengine ndugu wa Palestina. Nitakwenda hata kama itanigharimu maisha yangu. Maisha yetu hayana thamani zaidi ya yale ya ushindi au kifo cha kishahidi," aliwaambia wabunge hao ambao walikuwa wakimshangilia.

Alisisitiza katika hotuba yake kwamba Jerusalemu ni mji mkuu wa Palestina.

"Gaza ni yetu na hatutakubali pendekezo lolote linalolenga kuigawa," aliongeza.

Mahmoud Abbas, ambaye anaishi Ramallah, katika Ukingo wa Magharibi, aliwasili Uturuki Jumatano kwa mwaliko wa serikali ya nchi hiyo.

Katika ziara yake aliealikwa kuhutubia bunge kama majibu ya mwaliko uliotolewa na Bunge la Marekani kwa Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu.

Rais wa Uturuki, HYPERLINK "https://www.rfi.fr/sw/lebo/recep-tayyip-erdogan/" \t "_self" Recep Tayyip Erdogan, amelaani vikali mwenendo wa Israel katika vita vilivyochochewa na mashambulizi ya Hamas ndani ya Israel Oktoba 7, mwaka jana. Wakati huo huo, majadiliano ya usitishaji mapigano yalianza Alhamisi nchini Qatar.

Duru hiyo mpya ya mazungumzo inafanyika baada ya kutolewa wito na wapatanishi kutoka nchi za Qatar, Marekani na Misri.

**RFI**

# Bil. 1/- yatumika jengo la uchunguzi wa maradhi

**Neema Sawaka na Shaban Njia**

SERIKALI imekamilisha ujenzi wa jengo la uchunguzi kwa wagonjwa wilayani Kahama, mkoani Shinyanga na kuwaondolea wananchi adha ya kusafiri zaidi ya Km 900 kwenda Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dar es Salaam au zaidi ya Km 200 kufuata huduma hiyo katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando, jijini Mwanza.

Jengo hilo ambalo limekamilika na kuwekewa vifaa tiba vya kisasa, limegharimu Sh. bilioni 1.099 chini ya mkandarasi Suma JKT Contruction Co.Ltd ya Kanda ya Ziwa, usimamizi ukiwa chini ya Mhandisi wa Halmashauri kwa kutumia mfumo wa Force Account.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa jengo hilo jana kwa kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa mwaka 2024, Godfrey Mnzava, Daktari Bingwa wa Mionzi, Fredrick Malunde alisema ujenzi wake umetumia fedha kutoka serikali kuu pamoja na mapato ya ndani ya halmashauri hiyo.

Alisema jengo hilo limesaidia kuwaondolea adha wagonjwa kwa kusafiri umbali mrefu kwenda Hospitali za Rufani za Bugando, KCMC na Muhimbili kutafuta huduma za mionzi na kila mwezi walikuwa wakisafirisha wagonjwa 100 mpaka 125, hali ambayo ilikuwa ikiongezea gharama kubwa katika matibabu yao.

Dk. Malunde alisema Sh. bilioni 1.099 zimetumika kujenga jengo hilo la kisasa na kuanza kutoa huduma karibu na wananchi.

Bingwa huyo alisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 500 ni fedha kutoka serikali kuu na Sh. milioni 599.238 ni za mapato ya ndani ya halmashauri hiyo na sasa hakuna mgonjwa anayesafirishwa kwenda hospitali za nje kutafuta huduma hiyo.

"Tayari tumeanza kuhudumia wagonjwa ambao wengi wao wanatoka halmashauri za jirani za Msalala, Ushetu na baadhi katika ya mikoa ya Geita na Tabora, kwa siku tunahudumia wagonjwa 1,000 mpaka 1,300," alisema Dk. Malunde.

Mkazi wa Malunga, Sarah Jafari alisema awali walikuwa wanasafiri umbali mrefu kutafuta huduma ya mionzi Bugando, jijini Mwanza na ilikuwa inaongezea gharama katika matibabu yao kwa kuwa kuna wakati iliwalazima kukodi gari na kupeleka wagonjwa wao wenyewe kutokana na gari la wagonjwa lililopo kuwa na matumizi makubwa.

Kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Mnzava, alisema serikali imekuwa inaboresha huduma za afya kwa kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinapatikana kwa urahisi ili wananchi wasipate shida.

Aliwaelekeza watumishi wa afya kufanya kazi kwa kuzingatia misingi yao ya kazi na kutojihusisha na vitendo vya rushwa ambavyo vinakandamizi utu wa wagonjwa, na atakayebainika awajibishwe kwa mujibu wa sheria.

Mwenge huo wa Uhuru uliweka jiwe la msingi katika Hoteli ya Kifahari ya Yolanda ambayo inamilikiwa na mwekezaji wa ndani kutoka Manispaa ya Kahama, Nestory Makune.

Mnzava, akiweka jiwe hilo la msingi, alisema serikali inaendelea kuhimiza wawekezaji wa ndani kuwekeza kwa wingi ili kuongeza mapato ya ndani pamoja na ajira kwa Watanzania.

Mwekezaji huyo, Makune, aliishukuru serikali kwa kutoa fursa za uwekezaji katika miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kukuza uchumi wa nchi na kutoa ajira kwa Watanzania.

## Wakulima wauza mbaazi kwa bei ya 1,986/- kwa kilo

**Na Stevie chindiye,** TUNDURU

WAKULIMA wa Kijiji cha Mbesa, wilayani Tunduru, mkoani Ruvuma wameuza tani 2,978,420 za mbaazi kwa bei ya Sh. 1,986 kwa kila kilo moja.

Akitangaza bei zilizotolewa na wanunuzi waliojitokeza kununua mbaazi hizo, Makamu Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika wilayani Tunduru (TAMCU), Kaisi Makolela, alisema kuwa katika mnada huo, bei ya juu ilikuwa Sh. 2,040 na bei ya chini ilikuwa ni Sh. 1,950.

Meneja Mkuu wa TAMCU, Marcelino Mrope, alisema kuwa kupitia mnada huo chama hicho kiliweka sokoni zao hilo kulingana na bei za mnada.

Wakiongea kwa niaba ya wakulima wenzao, Hemed Said, Hussein Ndago na Zaituni Chilunfa, walisema bei iliyotolewa katika mnada huo inaridhisha, wakiwataka wanunuzi kuacha tabia za kupandisha minada ya kwanza na kishusha bei minada inayofuata, hali ambayo huwakatisha tamaa wakulima.

Diwani wa Mbesa uliko-fanyika mnada huo, Daniel Mlanda, alitumia nafasi hiyo kuwataka wakulima kutumia vizuri fedha watakazopata ili ziwaletee manufaa kiuchumi.



Mkazi wa Manzese, Dar es Salaam, Busara Maningi, akifanya muamala kupitia huduma mpya ya NBC Wakala Pesa, wakati wa uzinduzi mkoani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NBC yazindua huduma ya wakala kuchochea ujumuishaji wa kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imetambulisha rasmi huduma yake mpya ya wakala kupitia benki ambayo inaruhusu mteja asiye na akaunti ya benki hiyo kufanya miamala ya kifedha kwa kutumia kitambulisho chake cha taifa.

Huduma hiyo ya NBC Wakala Pesa ni sehemu ya azma ya benki hiyo katika kuwezesha na kuchochea ujumuishi wa kifedha nchini.

Uzinduzi wa huduma hiyo umefanyika juzi jijini Dar es Salaam katika moja ya Ofisi ya Wakala Mkuu wa benki hiyo eneo la Manzese, ukiongozwa na Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Wadogo na Wakubwa wa benki hiyo, Elibariki Masuke.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na maofisa wa benki hiyo, akiwamo Meneja wa Huduma ya Uwakala, Jacquilen Sindano.

Akizungumzia huduma hiyo, Masuke alisema inatoa nafasi kwa wateja wasio na akaunti kwenye benki hiyo au benki nyingine kuweka, kutoa na kuhamisha fedha kupitia wakala wa NBC walioidhinishwa kwa kutumia vitambulisho vyao vya taifa au vya ukaazi kwa upande wa Zanzibar.

"Kupitia huduma hii, NBC tunatambua kuwa upatikanaji huduma za kifedha ni haki ya msingi ya kila Mtanzania bila kujali hadhi zao za kijamii na kiuchumi.

"Huduma yetu ya 'NBC Wakala Pesa' imebuniwa kuvuka vikwazo ambavyo kwa muda mrefu vimekuwa vikizuia maelfu ya wananchi kutumia mfumo rasmi wa kifedha," alisema.

Aliongeza kuwa huduma hiyo bunifu pamoja na kurahisisha mchakato wa miamala pia inachochea idadi kubwa ya wananchi kushiriki katika huduma rasmi za kifedha.

"Uzinduzi wa huduma hii ni ushuhuda wa azma dhati ya NBC ya ujumuishaji wa kifedha. Kwa kutumia mtandao wetu mpana wa mawakala nchini, tunaleta huduma za benki moja kwa moja kwenye milango ya wale ambao kwa kihistoria hawakuhudumiwa," alisema.

Katika uzinduzi huo, ilishuhudiwa wateja wakipata fursa kujifunza huduma hiyo moja kwa moja huku wakionyesha shauku na kufurahia urahisi mpya uliopatikana.

"Nimekuwa mvivu kufungua akaunti ya benki kwa sababu ya kuhofia taratibu ndefu," alisema Fatuma Ally, mkazi wa eneo hilo.

"Lakini kupitia huduma hii ya 'NBC Wakala Pesa' sasa ninaweza kusimamia masuala yangu ya kifedha kwa urahisi bila kabla ya kufungua akaunti," alisema.

Akizungumzia huduma hiyo, Frank Maningi, Wakala Mkuu wa NBC Manzese, alisema huduma hiyo inatarajiwa kuleta mageuzi makubwa ya kihuduma kupitia benki kutokana na kugusa idadi kubwa ya w

Watanzania ambao hawajafungua akaunti za benki.

"Huduma hii ni mageuzi makubwa kwa jamii yetu. Inatoa njia salama na zaidi inajumuisha watu wengi zaidi kuingia katika huduma rasmi za kifedha, hatua ambayo itawawezesha kufanya miamala kwa urahisi," alisema.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa na maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosabisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-26

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"Sawa sasa tumejua kuwa tajiri Boniphace Materu ndiye kinara wa mauaji haya. Na yeye ndiye baada ya kufanikisha kutuma watu kumuua Mariamu akahonga baadhi ya madaktari kubadilisha uchunguzi wa kifo kwa sababu ya kuficha ushahidi, baada ya nguvu ya umma pamoja na wanandugu, uchunguzi wa kweli ukafanyika, lakini akabambikiwa muuaji mtu ambaye siye, naye ni wewe. Sasa kinachotakiwa hapa ni jinsi gani ya kufanya ili umma ujue kuwa Materu ndiye kinara wa mauaji." "Ni kweli afande kwa sababu mpaka sasa mimi ndiye natambulika kama muuaji."

"Kaka Shija, kuna nyaraka fulani ambazo zitakuwepo ofisini kwako, nazitaka kwa ajili ya ushahidi, nitakwambia ni za aina gani. Halafu kuna zingine zitakuwa ndani ya ofisi ya Materu. Tukizipata hizi tu, basi tutawabadilisha watu wote na kumwanika hadharani aliyesababisha mauaji ya Mariamu, lakini tukifanya pupa haitowezekana. Sisi wenyewe tutajua kuwa yeye ndiye injinia wa mauaji kwa sababu za kimapenzi, lakini kuwaaminisha watu kuwa tajiri yule ndiye muuaji na si wewe ni kazi ngumu, pia hata mahakamani utahitajika ushahidi usio na shaka hata kidogo." Afande Willy akatanabaisha. Willy na kaka yake dokta Shija wakapeana majukumu na kumtaka Kamal atulie, kwani kuna kazi moja kubwa atapewa ili kukamilisha ushahidi wa kumtia hatiani Materu, mfanyabiashara maarufu nchini, mwenye makampuni, maduka, gereji, na vitega uchumi mbalimbali nchini, lakini pia akiwa na mpango wa kuwania ubunge katika moja ya majimbo nchini.


"Nakuomba pia, nenda kachukua nguo zako na vitu vyako huko unakuishi, kwa siku hizi chache kabla ya kazi hiyo utakaa hapa." Afande Willy alimwambia Kamal, ambaye aliafiki.

Afande Willy alipendezwa sana na Kamal. Uwezo wake wa akili na mambo anayoyawaza na kuyafanya, yalimfurahisha na kweli kama alivyoambiwa na kaka yake Dokta Shija, yalifanana sana na askari wapelelezi.

Mara kwa mara baada ya kurejea kazini walifanya wote mazoezi uani, kwani afande Willy, alikuwa amenunua.

Alimwambia kuwa hakutakiwa kuwa fundi gereji, bali askari polisi tena mpelelezi. Alipoambiwa historia yake kuwa alikuwa akipenda sana kusoma vitabu vya kipelelezi, pamoja na filamu zake, hakushangaa.

"Kwa umri ulionao bado hujachelewa sana rafiki yangu." Mara kwa mara afande huyo huwa anamwambia, lakini Kamal huona kama anapewa moyo tu.




"Sasa rafiki yangu nataka nikupime kama wewe kweli unaweza kazi ya upelelezi." "Kwa vipi afande?" Akauliza Kamal siku moja baada ya kumaliza mazoezi na kukaa mezani wakila supu, mikate na mayai ya kuchemsha. "Kuna kazi ngumu kidogo nataka kuifanye, lakini kwa sababu nimekuangalia nimeona wewe utaiweza. Kama ingekuwa mwingine wala nisingemtumbukiza kwenye janga."

"Vyovyote vile mimi niko tayari kunipa misheni ya kwenda kuifanya." Akajibu Kamal. Afande Willy akacheka. "Hii ni kwa ajili ya wewe rafiki yangu. Kumbuka tunaifanya kazi hii kwa kujipa mamlaka sisi wenyewe. Tunafanya hivi kwa sababu siyo kukuokoa wewe ili asiende kuning'inizwa kitanzini kwa tuhuma za kumuua mpenzi wako Mariamu kimakosa, lakini pia kuuweka ukweli hadharani ambao umefichwa kwa sababu ya rushwa. Kwetu nchini rushwa ni adui wa haki. Lakini wenye pesa wamepenyeza pesa kuanzia hospitalini hadi kwenye Jeshi la Polisi kwa wale ambao si waaminifu ambao wamewaaminisha wananchi uongo. Wamewaaminisha mashetani wawe malaika na malaika kuwa mashetani." Akaongea Afande Willy kwa uchungu. Kabla Kamal hajaongea lolote akaendelea. "Nataka hata kama nikipata adhabu kwa kufanya kazi ambayo sikutumwa, lakini wananchi watambue ukweli wa hili upo wapi. Naweza kuhukumiwa na jeshi langu, lakini si na wananchi." "Mhh! Umeanza lini kuwa mwanasiasa?" Kamal aliuliza kwa utani, kabla ya wote wawili kuangua kicheko. Baada ya hapo mipango ikaendelea. Afande Willy akamkumbusha kuwa kaka yake Dokta Shija ameshakusanya baadhi ya vielelezo ambavyo waweza kuvitumia kwa ajili ya kumuweka hadharani kinara wa mauaji, hivyo Kamal naye akatumwa kazi ya kuifanya mahali ili kukamilisha ushahidi.

**Gereji zake zilizidi kupata wateja, akiwa na tenda ya kutengeneza mabasi ya kusafiri yanayomilikiwa na vigogo ambao hawakutaka majina yao yawekwe hadharani na hata wafanyabiashara wenzake.**

"Kuwa makini, nakuamini Kamal, najua wewe si askari, lakini ifanye kama afande kwa sababu umekaa kama afande na mbinu zote ulizozifanya kuwakimbia askari wasikukamate hata mimi nimekuvulia kofia, ndiyo maana nimekuamini." "Kwa sababu umesema niko kama afande, mimi ndiyo mhusika ambaye anatuhumiwa na mauaji, na namsaka muuaji wa mpenzi wangu, ambaye amenigeuzia kibao. Nitaifanya kazi hii kwa umaridadi mkubwa na hutaamini." Afande Willy alicheka, akampa mkono. Wakashikana mikono ishara kuwa wamekubaliana na hicho kitakachokwenda kufanyika.

****************************

Akiwa kwenye ofisi yake karibu na eneo la Makumbusho jijini Dar es Salaam, Boniphace Materu aliendelea kuvuta sigara zake mfululizo.

Kila kitu alichokifanya aliona chema. Utajiri wake ulizidi kuongezeka. Makampuni yake yaliendelea kuzalisha faida, wakati mwingine tofauti na alivyofikiria.

Gereji zake zilizidi kupata wateja, akiwa na tenda ya kutengeneza mabasi ya kusafiri yanayomilikiwa na vigogo ambao hawakutaka majina yao yawekwe hadharani na hata wafanyabiashara wenzake.

Mpango wake wa kuwania ubunge katika moja ya jimbo mkoani Kilimanjaro alikozaliwa nao ulikuwa ukiendelea vizuri. Alijiona mwenye bahati kwenye ulimwengu huu.

Siku yake ya mkononi iliita. Baada ya kuona jina alitabasamu kidogo, halafu akaweza sikioni. "Niambie."

"Mkuu naomba unitumie milioni mbili kwa ajili ya kulainisha baadhi ya wapigakura. Unajua wanakukubali sana, sema unajua tena wanataka chochote kitu. Hili jimbo ni lako tu mkuu." Sauti ilisikika upande wa pili.

Huyo alikuwa ni mpambe wake aliyemweka kuhakikisha anafanya kila njia, wananchi wa jimbo hilo wanamchagua yeye kuwa mbunge mwakani.

"Haina neno, kuna kazi hapa naifanya, nikimaliza nitakucheki. Nitaitumia kwenye simu yako. Wewe fanya kazi, yaani nipata ubunge wewe mwenyewe utafurahi." Waliongea kiasi cha dakika mbili hivi hadi pale waliporidhika kuwa wameelewena.

Ni kweli Materu pamoja na utajiri wake alikuwa anataka ubunge ili kuendelea kujijengea heshima. Ana kila kitu, utajiri wa pesa, viwanda, makampuni, mahoteli, gereji, kwa sasa alichohotaji ni kinga ya uheshimiwa.

**Itaendelea Jumamosi**

# KLABU TISA KAMILI KUWANIA TAJI LA CECAFA WANAWAKE

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU tisa zinatarajia kushiriki katika mashindano ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake (CECAFA), yanayotarajiwa kufanyika kuanzia leo hadi Agosti 31, mwaka huu jijini Addis Ababa, Ethiopia.

**Ofisa Mtendaji Mkuu wa CECAFA, Auka Gecheo, aliliambia gazeti hili jana timu zote tisa zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo kati ya nchi wanachama 12 zimewasili Addis Ababa tayari kuanza kuchuana.**

Gecheo alisema anaamini mashindano ya mwaka huu yatakuwa na ushindani zaidi kwa sababu kila timu inahitaji kupata tiketi ya kushiriki fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika zitakazofanyika baadaye mwaka huu.

Alizitaja timu hizo ni pamoja na wenyeji CBE, Polisi Kenya, Yei Joint FC (Sudan Kusini), Warriors Queens (Zanzibar) na Rayon Sport kutoka Rwanda ambazo zimepangwa katika kundi A huku kundi B likijumuisha Simba Queens (Tanzania), PVB Buyenzi (Burundi), Kawempe Muslim (Uganda) na FAD Djibouti.

"Kila kitu kinakwenda vizuri, tunatarajia kuwa na mashindano yenye ubora na kiwango cha juu, tumekuwa na ushindani kila mwaka katika mashindano ya wanawake, tunajivunia uwakilishi mzuri wa timu za wanawake katika michuano mbalimbali wanayopata nafasi ya kushiriki," Gecheo alisema.

Mechi ya ufunguzi katika mashindano hayo inatarajiwa kuwakutanisha CBE dhidi ya Rayon Sports wakati mapema mchana Polisi ya Kenya watavaana na Warriors Queens.

Simba Queens yenyewe itaanza kampeni ya kuwania ubingwa wa mashindano hayo kesho kwa kukutana na FAD ya Djibouti huku mchezo wake wa pili ukitarajiwa kufanyika Jumanne dhidi ya Kawempe Muslim na itamaliza mechi za hatua ya makundi Agosti 22, mwaka huu kwa kuikabili PVB Buyenzi.

Timu mbili zitakazomaliza katika nafasi mbili za juu zitatinga hatua ya nusu fainali, na fainali ya mashindano hayo zitafanyika Agosti 31, mwaka huu.



Wachezaji wa Simba Queens wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati kwa Wanawake dhidi ya FAD Djibouti itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Abebe Bikila jijini Addis Ababa nchini Ethiopia. **PICHA: SIMBA SC**

# Uchaguzi TWFA mambo yameiva

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Uchaguzi ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imetangaza majina ya wagombea nane waliopita katika mchujo wa awali kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Nchini (TWFA), utakaofanyika Septemba 14, mwaka huu mkoani Kilimanjaro.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya TFF, Benjamin Kalume, aliwataja wagombea hao ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TWFA, Somoe Ng'itu na Amina Karuma wanaowania nafasi ya mwenyekiti.

Kalume aliwataja wagombea wengine waliopita katika mchujo huo wa awali ni Zena Chande, Fatuma Selemani na Veronica Samo ambao watachuana kuwania nafasi ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF.

Aliongeza wagombea wanaowania Ujumbe wa Kamati ya Utendaji ya TWFA ni Irene Ishengoma, Mwanaheri Kalolo na Ndinagwe Sungura.

"Kwa mujibu wa katiba yao, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF anatakiwa mmoja na Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya TWFA wakuchaguliwa wanatakiwa wawili tu," Kalume alisema.

Aliongeza usaili wa wagombea umepangwa kufanyika Agosti 22, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

TWFA inafanya uchaguzi wake baada ya kukamilisha mchakato wa kusajili katiba yake pamoja na za wanachama wake lakini pia ikishindwa kupata viongozi wa juu katika uchaguzi uliofanyika mwaka 2021 jijini Tanga.

Nafasi ambazo hazikupata viongozi katika uchaguzi uliopita baada ya kura zao kuzidi idadi ya wajumbe ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Katibu Msaidizi.

# Mashujaa, Dodoma Jiji FC mechi ya kisasi

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mashujaa FC na Dodoma Jiji ambazo zilicheza mechi za mwisho za kufunga dimba la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita zinakutana leo katika mechi ya raundi ya kwanza msimu huu itakayochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani Kigoma.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana Mei 28 katika mchezo wa kufunga msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, wenyeji Mashujaa wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0.

Miezi miwili na siku kadhaa, timu hizo zinakutana tena kwenye uwanja huo huo katika mechi yao ya kufungua msimu wa 2024/24.

Mashujaa itaingia uwanjani ikiwa na kocha yule yule wa msimu uliopita, Mohamed Abadallah 'Bares' ambaye amesema kikosi chake kiko tayari si tu kwenye mchezo wa leo, bali kwa ajili ya msimu mzima wa Ligi Kuu Bara.

"Tuko tayari, tumekuwa tukijiandaa na msimu mzima wa ligi na si mechi moja, hivyo tunawasubiri Dodoma Jiji ili tuone tunakabiliana nao vipi kama ilivyokuwa msimu uliopita," alisema Bares.

Dodoma Jiji msimu huu inafundishwa na Mecky Maxime, badala ya Mkenya Francis Baraza kama ilivyokuwa msimu uliopita walipokutana.

Maxime ameliambia gazeti hili kutokana na usajili uliofanyika, ana imani watatoa ushindani mkali si kwa Mashujaa FC, bali kwa timu yoyote inayoshiriki ligi hiyo ya juu Tanzania Bara.

"Tumefanya usajili mzuri wa wachezaji ambao ni wazoefu kwenye Ligi Kuu, kwa hiyo tunakwenda kucheza mechi dhidi ya Mashujaa tukiwa hatuna presha kwa sababu wachezaji wengi wana ukomavu kwenye ligi hii," alisema Maxime.

Moja ya kitu ambacho mashabiki wa soka watakishuhudia leo, ni straika wa zamani wa Mashujaa, Reliants Lusajo, ambaye alifunga mabao mawili dhidi ya Dodoma Jiji yaliyoisaidia timu hiyo kubaki Ligi Kuu, leo akiwa upande wa pili.

Dodoma Jiji waliamua kumsajili Lusajo, baada ya kuwasumbua na kuwapiga mabao mawili katika mechi hiyo.

Baadhi ya wachezaji wa Mashujaa wapya watakaonekana katika mchezo wa leo ni Seif Karihe, Chrispin Ngushi, Abdulmalik Zacharia, Mohamed Mussa, Carlos Protus, Mathew Michael, Ismail Mgunda, Robert Mathias na Ally Nassor 'Ufudu' huku Dodoma Jiji mbali ya Lusajo pia itawategemea nyota wake wapya akiwamo Waziri Junior, Ibrahim Ajibu, Heritier Lulihoshi, Daudi Milandu, Dickson Mhilu na Allain Ngeleka.

Mechi nyingine ya ligi hiyo leo itachezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi kwa Namungo kuwakaribisha Fountain Gate kutoka Dodoma.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ERIKSEN RUKSA KUONDOKA

MANCHESTER United imemwambia kiungo wa kimataifa wa Denmark, Christian Eriksen, mwenye umri wa miaka 32, yuko huru kutafuta klabu mpya mwezi huu na anaweza kuondoka kwa mkataba wa bei nafuu. (***Football Insider***)

### UNITED YAMKATAA DE JONG

KLABU ya Manchester United haina mpango wa kumnunua kiungo wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 27.(***Metro***)

### ATLETICO KUMUUZA FELIX

ATLETICO Madrid inalenga kukamilisha mauzo ya mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Felix, mwenye umri wa miaka 24 na kumsajili kiungo wa kati wa The Blues, Conor Gallagher (24), ifikapo Jumatano. (***AS***)

### FOFANA AKARIBIA MILAN

AC Milan imefikia makubaliano na Monaco kwa ajili ya kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Youssouf Fofana, mwenye umri wa miaka 25, ambaye ananyatiwa na Manchester United. (***Anga Italia***)

### BERGE ATAJWA UNITED

MANCHESTER United inaendelea kujadiliana na Burnley kuhusu mkataba wa kiungo wa Timu ya Taifa ya Norway, Sander Berge, mwenye umri wa miaka 26. (***Sky Sports***)

### JOHNSTON AGEUKA LULU

KLABU za Stoke City, Swansea City na Oxford United zimeonesha nia ya kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya Scotland, Max Johnston, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Sturm Graz. (***Football Insider***)

### ARCHER SOKONI ULAYA

UNION Berlin na Getafe zinaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa England, Cameron Archer, mwenye umri wa miaka 22 kwa mkopo kutoka Aston Villa. (***Fabrizio Romano***)

### CHELSEA KUMUUZA MADUEKE

CHELSEA imeweka bei ya pauni milioni sita kwa klabu yoyote inayotaka kumsajili winga wa England, Noni Madueke, mwenye umri wa miaka 22. (***Athletic***)

### ALONSO AITAMANI UNITED

MLINZI wa zamani wa Chelsea na Hispania, Marcos Alonso, mwenye umri wa miaka 34, angependa kujiunga na Manchester United baada ya kuwa mchezaji huru anapoondoka Barcelona. (***Fabrizio Romano via Givemesport***)

### PSG YAVUTIWA NA DOUE

PARIS St-Germain iko tayari kuipiku Chelsea katika mbio za kumsajili kiungo wa klabu ya Rennes ya Ufaransa chini ya umri wa miaka 23, Desire Doue. (***ESPN***)

### BOSCAGLI ANUKIA BRIGHTON

KLABU ya Brighton imewasilisha ofa iliyoboreshwa kwa mlinzi, Olivier Boscagli mwenye umri wa miaka 26 ambaye aliichezea timu ya vijana ya Ufaransa, lakini bado inaonekana kutoafikiwa na PSV Eindhoven. (***Voetbal International***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: UBINGWA EPL 2024/25 WA ARSENAL

**LONDON,** England

**Kocha huyo atamba ameboresha kikosi chake na kila mchezaji...**

MIKEL Arteta anaamini Arsenal wamepiga hatua kubwa kufikia lengo lao la kunyanyua taji la Ligi Kuu England (EPL), msimu huu.

Washika bunduki hao wataanza kampeni yao ya Ligi Kuu England ya msimu wa 2024/25 leo wakiwakaribisha Wolverhampton Wanderers.

Wana zaidi ya miongo miwili hawajabeba taji hilo, na wanatarajia kuwaondoa mabingwa watetezi Manchester City kutoka kileleni na kutwaa taji hilo linalotamaniwa sana msimu huu.

Kocha wa Arsenal, Arteta anajiamini katika uwezo na amesema timu yake imefanya kazi kwa bidii katika maandalizi ya msimu huu.

"Pia, tuko tayari kufanya vyema na kuleta mataji makubwa, lakini itahusu safari na tunapaswa kufikiria kuanzia ambapo tunataka kuwa siku ya kwanza," alisema kocha huyo wa kutoka Katalunya Hispania akiiambia Sky Sports.

"Nadhani tulikuwa na maandalizi mazuri ya msimu mpya, tumepiga hatua kubwa na tuko tayari kwenda.

"Ili kuboresha namba hizo matokeo ya msimu uliopita inakuwa ngumu sana, lakini hiki ndicho kiwango kinachohitajika kushinda Ligi Kuu. Kila mwaka itakuwa ngumu zaidi, kwa hiyo lazima tufanye vizuri zaidi, lazima tutafute nafasi katika maeneo kabla hatujachunguza na sote tunapaswa kuweka viwango vipya na tukifanya hivyo tutajipa nafasi nzuri sana.

"Kuna maeneo fulani ya timu ambayo unaweza kuboresha kila wakati, lazima urudi nyuma na uhisi hali ya joto, uhisi timu inahitaji nini? Tunakosa nini?

"Tumeweka mambo mengi katika kipindi hiki cha joto ili kuifanyia mabadiliko timu na kupata kiwango cha juu ndani ya timu hii ili kuwatia moyo wachezaji, nadhani wachezaji wanatakiwa waje kuona kitu kipya, kitu ambacho ni tofauti. Tuna wachezaji ambao wana uwezo wa kuwapa moyo wachezaji, wanauwezo na ubora wa hali ya juu, wana uwezo wa kufundisha, wanautaka sana, ni wachanga, wanataka kufanya hivyo."

Arsenal hadi sasa imemsajili beki wa kati wa Italia, Riccardo Calafiori, katika dirisha la usajili la kiangazi.

# NAPOLI WAJITOSA KUMWANIA MCTOMINAY




**NAPLES,** Napoli

NAPOLI ipo katika mazungumzo na Manchester United kuhusu uwezekano wa kumsajili, Scott McTominay, lakini wangependelea kumchukua kwa mkopo badala ya uhamisho wa kudumu, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland alifunga mabao 10 katika michuano yote msimu uliopita, ikiwa ni pamoja na magoli ya kufutia machozi katika ushindi wa Ligi Kuu England dhidi ya Brentford na Chelsea, na alikuwa akifuatiliwa na Fulham mapema katika dirisha la majira ya joto.

Hata hivyo, Cottagers hao walikatishwa tamaa na bei ya Mashetani Wekundu ambayo ilikuwa karibu na Euro milioni 30 na ada hiyo pia inatarajiwa kuwa nje ya uwezo wa Napoli.

Gazeti la Times limefichua mabingwa hao wa Serie A msimu wa 2022/23, ambao sasa wapo chini ya Kocha, Antonio Conte, wangependa kumchukua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 kwa miezi 12 ijayo.

Conte alijiunga na Napoli mwanzoni mwa msimu wa joto, lakini tayari amefichua kusikitishwa kwake na dirisha la usajili la majira ya joto kuwa la polepole hadi sasa, akisema: „Nilijiweka kamili katika klabu hii, nilijua hali niliyoipata na sokoni kuna vikwazo katika suala zima la gharama ya mchezaji au mshahara.

"Wachezaji wengi hawaji hapa kwa sababu hatuchezi katika mataji ya Ulaya. Naitakia Napoli kuwa bora na kujaribu kuimarisha kikosi kwa sababu tunakihitaji. Halafu sijui nini kitatokea."

Fulham waliachana na mpango wa kumnunua McTominay baada ya ofa ya pauni milioni 20 kukataliwa, lakini Kocha wa United, Erik ten Hag hapo awali alifichua nia yake ya kutaka kumbakisha kiungo huyo.

Alisema wakati wa maandalizi ya msimu: „Unapofunga mabao 10 kwa msimu mmoja na kufanya vizuri sana kwa Scotland, basi kutakuwa na maslahi, lakini tunataka kumbakisha kwa sababu ni mchezaji muhimu sana kwa kikosi chetu."

# Enrique akerwa, amtakia heri Mbappe

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Paris Saint-Germain, Luis Enrique, alimjia juu mwandishi wa habari kwa kumuuliza kuhusu Kylian Mbappe, ambaye aliihama klabu hiyo ya Ufaransa mwishoni mwa msimu uliopita na kujiunga na Real Madrid kwa uhamisho huru.




Mbappe alifunga bao la kwanza kwa Madrid Jumatano usiku, na kuchangia ushindi dhidi ya Atalanta wakati timu yake mpya ikinyakua taji la UEFA Super Cup.

Enrique alipokuwa akizungumza na vyombo vya habari kabla ya mechi ya kwanza ya PSG ya Ligue 1 dhidi ya Le Havre juzi Ijumaa usiku, mwandishi wa Hispania, kwenye kundi la wanahabari aliuliza kuhusu kumkosa Mbappe kwenye kikosi chake msimu huu.

„Jinsi gani Wahispania hawa wanavyochosha," lilikuwa jibu la kufoka la Enrique.

„Sikufikiri kama watu wangeniuliza tena kuhusu Kylian. Sijawahi kuwa na tatizo na Kylian, namtakia heri yeye na mdogo wake, Ethan. Lakini ninatumaini Madrid itapoteza ikicheza dhidi yetu."

Baada ya kusaini mkataba mpya wa miaka miwili na PSG mnamo 2022, Mbappe alimaliza mkataba wake na kuwa mchezaji huru ilipofika Juni mwaka huu.

Tayari alikuwa amewasiliana na PSG, hakukusudia kuongeza muda tena baada ya hapo na alijiunga rasmi na Madrid bila ada ya uhamisho mwezi uliopita.

PSG ilikubali ofa ya rekodi ya dunia ya euro milioni 300 kutoka kwa Al Hilal mnamo 2023, ambayo ingewawekea fedha nyingi mchezaji ambaye amebakiza mwaka mmoja tu kwenye mkataba wake.

Lakini Mbappe, ambaye tayari alionekana kutaka kujiunga na Madrid alikataa hata kukutana na klabu hiyo ya Saudi Pro League.

Mbappe atacheza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakati Madrid watakaposafiri kwenda Mallorca hapo kesho.

# Walker atamba City itatwaa tena ubingwa

**MANCHESTER,** England

NAHODHA wa Manchester City, Kyle Walker amesema ubingwa wa Ligi Kuu ya England ni wao, huku timu yake ikitarajia kushinda taji la tano mfululizo, jambo ambalo halijawahi kushuhudiwa.

City ilikuwa klabu ya kwanza kushinda taji mara minne mfululizo katika Ligi Kuu England msimu uliopita na wataanza kutetea taji hilo kesho watakapoifuata Chelsea.

Akizungumza na BBC Radio 5 Live, beki huyo wa pembeni wa England, Walker alisema: „Sisemi ni kujisifu, lakini tumeshashinda mara nne mfululizo - hili ni kombe letu. Ninaweza kukwambia, unapotazama kwenye mkono wako na una beji ya dhahabu ambayo hakuna mtu mwingine anayo, unapata hisia nzuri."

Chini ya Pep Guardiola, City imekuwa mashine ya kushinda bila huruma. Walker amesema: „Kuchukua ubingwa mara nne mfululizo, huku tukiwa tumechukua makombe matatu katika msimu mmoja, ni mafanikio makubwa. Na kwenda tena na kushinda Kombe la Super Cup na Klabu bingwa ya Dunia.

„Sasa, kipi kitukwamishe kushinda mara tano mfululizo? Kwa nini tusifanye kitu ambacho hakitakuja kufanyika tena? Hiyo ndiyo motisha tunayopaswa kuwa nayo kama wachezaji, na mimi kama nahodha."

Walker anakiri kuwa klabu hiyo inataka „mafanikio ya papo hapo - na hilo ndilo tunalopaswa kulitekeleza".

„Nadhani kama huna njaa ya ushindi, Guardiola hawezi kuwa nawe kwenye klabu. Ushindi ni sehemu kubwa ya vinasaba vyake."

„Angalia timu alizoondoka na kuzisimamia, wachezaji aliofanya nao kazi. Haoni aibu kukwambia usipofanya vizuri."



# Ateba awaita, Simba ikiikabili Tabora...

INATOKA UK. 24

zichezea timu mbalimbali ikiwamo PWD Bamenda, Dynamo Douala za Cameroon na USM Alger pamoja na kikosi cha Timu ya Taifa ya Cameroon maarufu Indomitable Lions.


Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema jana walikuwa na machaguo mengi lakini kura ya 'ndio' ikamwangukia Ateba.

"Tumemsajili Ateba kutokana na kiwango alichonacho, hatukumtoa nyumbani, tumemtoa kwenye timu yake ya USM Alger na alikuwa tayari amefanya mazoezi ya utimamu wa mwili na kikosi chake, alikuwa anataka kujiandaa na majukumu mapya, sisi tukamchomoa, tumemnunua kwa fedha nyingi na hatimaye ametua kwa mkataba wa miaka miwili.

Mimi nina imani naye na mashabiki wa Simba nadhani nao wana imani naye, na niwaambie tu, moja kwa moja anaingia kwenye kikosi, hahitaji mazoezi ya peke yake, hata kesho (leo), anaweza kupewa jezi na akacheza," alisema Ahmed.

Akiwa kwao Cameroon, alifunga mabao 40 katika michezo 48, kabla ya kuhamia Algeria kwenye klabu yake mpya, ambako amefunga magoli matatu na kutoa 'asisti' 11.

Nyota huyo anapishana na Willy Onana, ambaye Simba imemuuza kwa klabu ya Al Hilal Benghazi ya Libya baada ya kukubali dau walilowatajia.



# COASTAL UNION KUWEKA REKODI MICHUANO CAF

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya miaka 35, kwa mara ya kwanza Coastal Union inashuka uwanjani leo kucheza mchezo wa mashindano ya kimataifa wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya wenyeji, Bravos do Maquis ya Angola.

**Mechi hiyo ya mkondo wa kwanza hatua ya awali itachezwa kuanzia saa 12:00 jioni kwa saa za Tanzania kwenye Uwanja wa Tundavala uliopo Lubango.**

Mara ya mwisho Coastal Union kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ilikuwa ni mwaka 1989, baada ya kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara wa mwaka 1988.

Akizungumza kutoka Angola, Ofisa Habari wa Coastal Union, Abbas El Sabri, alisema walifika salama nchini humo, na hawajakutana na chochote ambacho kingeweza kuwakwaza katika mchezo huo, hivyo amewataka Watanzania kuwaombea wachezaji wawe salama kwa ajili ya kuipambania nchi.

"Hatuchezi kama Coastal Union pekee, bali tunaiwakilisha nchi, ushindi wowote au kufanya vizuri ni sifa kwa nchi yetu, hivyo tuko tayari na wachezaji wetu wana morali kubwa," alisema Sabri.

Kocha Mkuu wa Coastal Union, David Ouma, alisema ingawa hawawafahamu vizuri wapinzani wao, lakini wamejipanga kucheza kwa uangalifu hasa kipindi cha kwanza ili 'kuwasoma'.

"Mpira ni ule ule tu, ila ni lazima uwe na angalau rekodi za uchezaji wa wapinzani wako, sijawaona, siwafahamu vizuri, lakini nitacheza kwa uangalifu kipindi cha kwanza, baada ya hapo nitakuwa nimepata picha ni nini nifanye kipindi cha pili, ila mechi ya marudiano hapa nchini tabu itawapata," alisema kocha huyo raia wa Kenya.

Mchezaji wa timu hiyo, Charles Mfuko, alisema kwa maandalizi waliyofanya, wana matumaini ya kwenda kushinda mchezo huo wa ugenini.

"Tumefanya maandalizi mazuri, Watanzania watuamini kuwa tunataka kufanyia kazi kwenye mechi hii ya kimataifa kwa sababu pia sisi ni wawakilishi wa nchi," alisema mchezaji huyo.

Naye Cosmas Lewis, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo alisema wana matumaini makubwa ya ushindi na haijalishi kama wanacheza ugenini.

"Tuna matumaini makubwa ya ushindi kwa sababu mpira ni ule ule tu, tutapambana kuhakikisha tunashinda," alisema Lewis.

Coastal Union na Waangola hao watarudiana Agosti 25, mwaka huu kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.



Wachezaji wa mpira wa kikapu wenye ulemavu kutoka sehemu mbalimbali jijini wakifanya mazoezi kwenye Uwanja wa JKM Park, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Awesu atua rasmi Simba SC

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI mabosi wa Simba wakisema wamefanya biashara nzuri kwa kumuuza kiungo mshambuliaji wake, Andre Willy Esomba Onana, rasmi kiungo Awesu Awesu ni mali ya Wekundu wa Msimbazi.

Juzi Simba ilitangaza rasmi imemuuza Onana kwenda klabu ya Al Hilal Benghazi ya Libya, nyota huyo alijiunga kwa Wekundu wa Msimbazi msimu uliopita na kupewa mkataba wa miaka miwili.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema 'biashara' ya mchezaji huyo imekamilika baada ya klabu hiyo ya Libya kufikia bei waliyokuwa wakiitaka.

"Onana amejiunga na Al Hilal Benghazi ya Libya baada ya pande zote kufikia makubaliano ya biashara, klabu tunamshukuru Onana kwa muda wote aliokuwa na sisi na tunamtakia kila heri katika maisha yake mapya ya soka ndani ya klabu hiyo," alisema Ahmed.

Onana alijizolea umaarufu baada ya kufunga magoli mawili katika mechi ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi Wydad Casablanca iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa msimu uliopita.

Aliongeza Simba pia imemalizana na KMC na kwa sasa rasmi kiungo, Awesu Awesu ni mali ya klabu yao.

"Uongozi wa klabu ya Simba unapenda kuujulisha Umma kuwa Simba na KMC zimefikia makubaliano hivyo mchezaji Awesu Ally Awesu ni mchezaji halali wa klabu yetu," alisema Ahmed.

Naye Mwenyekiti wa KMC, Herry Misinga, alithibitisha mchezaji huyo kujiunga na Simba baada ya pande zote hizo mbili kufikia makubaliano.

"Ni kweli tumemalizana na Simba, wamefuata taratibu na tumeafikiana, Awesu ni mali ya Simba, sisi KMC tunamtakia kila la heri," Misinga alisema.

# *Yanga uwanjani ikiwaza taji CAF*

INATOKA UK. 24

waingie woga.

"Tunajua Yanga ni timu nzuri na tunajua msimu uliopita walifika hatua gani, ilikuwa ni robo fainali, lakini haitutii woga kwa sababu nao wana udhaifu wao ambao tumeuona katika michezo yao, tutaitumia kuwaadhibu," Parris alisema.

Aliongeza wachezaji wake wana morali ya hali ya juu na wako tayari kukutana na wapinzani wao huku akisema kila mmoja 'anautaka' mchezo huo.

"Mechi itakuwa ngumu na yenye upinzani mkubwa kutokana na ubora wa timu zote mbili. Lakini kikubwa kinachotakiwa ni utulivu wa kutumia nafasi pale itakapotengenezwa," alisema kocha huyo raia wa Burundi.

Kocha huyo pia aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Shirikisho la Soka Nchini (TFF) kwa kuwakubalia kucheza michezo yao Dar es Salaam.

Nahodha wa Vital'O, Ndayishimiye Hussein, alisema wamefanya maandalizi mazuri na kwa sababu hiyo anaamini watafanya vyema na wanachokisubiri kwa sasa ni muda wa mchezo.

"Malengo yetu ni kupata pointi tatu, tunataka tuwaonyeshe wapinzani wetu wanaweza kufungwa kama zinavyofungwa timu nyingine," alisema nahodha huyo.

Aliongeza kikosi chake kinaundwa na wachezaji watano kutoka nje ya Burundi wenye uzoefu na mashindano ya kimataifa ambao anaamini watasaidia kupata matokeo chanya.

**Imeandaliwa na Somoe Ng'itu, Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

Michezo
Nipashe
Jumamosi Agosti 17, 2024



Walker atamba City itatwaa tena ubingwa UKURASA 22

# Yanga uwanjani ikiwaza taji CAF

●●● Gamondi ataka ushindi mnono leo ikiikabili Vital'O, hata hivyo...

**Na Waandishi Wetu**

MABINGWA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wanatarajia kukutana na Vital'O kutoka Burundi katika mechi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kuanzia sa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

**Vital'0 ndio wenyeji wa mechi hiyo baada ya kukosa uwanja wenye sifa ya kutumika katika michuano hiyo inayosimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF) huko nyumbani kwao.**

Kuelekea mechi hiyo, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema msimu huu wanataka kuchukua kila kikombe cha mashindano ambayo watashiriki lakini akisisitiza ikiwamo ubingwa wa Afrika.

Hersi alisema Yanga wanahitaji kutwaa taji hilo na wala si kufika hatua ya robo au nusu fainali ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka.

Rais huyo alisema kikosi walichonacho msimu huu kina uwezo wa kubeba kombe hilo kubwa Afrika.

"Kila mashindano ambayo tunashiriki safari hii dhamira yetu ni kubeba kombe, tunaweka mguu katika mechi za Ligi ya Mabingwa, dhamira kubwa na kwa baraka za Mwenyezi Mungu kwa nini tusiwe timu ya kwanza Tanzania kuleta ubingwa wa Afrika?" alisema Hersi.

Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, aliliambia gazeti hili mechi hiyo haitakuwa rahisi kama ambavyo wengi wanafikiria, lakini amezungumza na wachezaji wake jinsi gani ya kufanya na hasa kutumia vizuri nafasi za kufunga mabao zitakazopatikana ili kuondoka na ushindi.

Gamondi alisema matokeo ya ushindi yatawaweka katika nafasi salama zaidi kuelekea mchezo wa marudiano.

"Tunataka kucheza vizuri na kushinda vizuri pia, ili tusiwe na presha sana katika mechi inayofuata, tunataka mchezo unaofuata uwe rahisi, nadhani hili ndilo kubwa zaidi," alisema kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Vital'O, Sahabo Parris, alisema pamoja na kwamba anaifahamu Yanga kuwa timu nzuri na yenye wachezaji wazoefu, lakini hawaihofii.

Parris alisema amekiona kikosi cha Yanga kilipocheza dhidi ya Simba na Azam hivi karibuni, hivyo amejiandaa vyema kukabiliana nao.

"Mechi huwa hazifanani, msidhani jinsi nilivyojipanga dhidi ya Pamba Jiji katika tamasha la Pamba Day, ndivyo nitakavyojipanga dhidi ya Yanga. Nipo hapa kwa wiki nzima, nimeona mechi ya Simba na Azam, zote zikicheza dhidi ya Yanga, nimeona zilikuwa zinakosea wapi, kwa hiyo mimi nimeyafanyia kazi mapungufu ya timu hizo zilipocheza dhidi ya mpinzani wangu, niseme tu tumejipanga kisawasawa kwa mechi hii," alisema kocha huyo.

Hata hivyo alikiri Yanga ina kikosi kizuri na chenye wachezaji wenye vipaji, lakini hayo yote hayawafanyi

INAENDELEA UK. 23



Pacome

## Ateba awaita, Simba ikiikabili Tabora Utd

**Na Adam Fungamwango**

MUDA mfupi tu baada ya kutambulishwa, straika, Christian Ateba, kutoka USM Alger ya Algeria, amewataka wanachama na mashabiki wa Simba kujitokeza kwa wingi kushuhudia ubora wake wakati wakiivaa Tabora United katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa KMC, Dar es Salaam.

Ateba ambaye amekamilisha kikosi cha Simba baada ya dirisha la usajili kufungwa rasmi hapo juzi usiku aliliambia gazeti hili kuwa, mashabiki wa timu hiyo hawataondoka na majonzi.

Ateba alisema yeye ni mshambuliaji wa kimataifa wa Cameroon, na amekuja katika timu ya Simba kufanya kazi aliyotumwa.

"Jina langu ni Ateba, mimi ni mshambuliaji wa kimataifa wa Cameroon, ni mchezaji mpya wa Simba, tutaonana katika mechi dhidi ya Tabora United, nawaomba wanachama na mashabiki wote waje uwanjani kuangalia nini tunafanya, nitakuwepo katika mechi hiyo na hawataondoka kwa majonzi, badala yake watafurahi," alitamba straika huyo.

Ateba ambaye ana umri wa miaka 25 ametua kwa Wekundu wa Msimbazi baada ya mabosi kufuata pendekezo la Kocha Mkuu, Fadlu Davids, aliyeweka wazi anahitaji kupata mshambuliaji mwingine ili kuongeza nguvu katika kikosi chake baada ya kuonekana kutoridhishwa na nyota waliopo.

Straika huyo amewahi ku-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002